FONOLOJIA YA NOMINO-MKOPO ZA KIKAMBA KUTOKA KISWAHILI

MAGDALENE NDANYA MULWA

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

NOVEMBER, 2014

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi…….Tarehe……..

MAGDALENE N. MULWA

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi……Tarehe……..

DKT. IRIBE MWANGI

Sahihi…….Tarehe…….

PROFESA P. MAINA MATU

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa:

Babangu, Marehemu Joseph Mulwa na mamangu Jemimah Nzila. Mapenzi yenu kwa elimu yalinitia shime.

Mpenzi mume wangu Simon Mbala, kwa upendo na stahamala; sahibu tumevuka pamoja.

Wanangu wapendwa, Victor, Gideon na Michael; nilijitahidi niwe kielelezo kwenu.

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwezo wa kuendeleza masomo yangu. Neema yake kuu imeniwezesha; “Ebeneza!” Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu, Profesa P. M. Matu na Daktari Iribe Mwangi kwa kuniongoza, kunielekeza na kuihakiki kazi yangu. Nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili kwa kujitolea kwa hali na mali kunifunza; Mungu awabariki. Nawatolea shukrani wanafunzi wenzangu wa uzamili kwa ushirikiano wenu kwa muda tuliosoma pamoja.

Nachukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa mume wangu Simon Mbala kwa kujitolea na kunihimiza wakati wote kusoma na kuandika kazi hii. Pia nawashukuru wanangu Victor, Gideon na Michael kwa kuvumilia sana nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Sitawasahau dada zangu Matilda na Grace kwa wema mlionitendea nilipokuwa nikisomea mjini; Mungu awabariki. Elizabeth Wanza, mchango wako katika maisha yetu kama familia nilipokuwa chuoni ni wa kukumbukwa.

Kufanikiwa kwangu katika kuhitimisha kazi hii kumetokana na juhudi za watu wengi lakini kwa sababu ya kubanwa na wakati na nafasi, sitaweza kuwataja wote. Kwa hivyo, ningependa kuwashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kwa kuwa msaada wenu ulinifaa; Mungu wa rehema awabariki nyote.

IKISIRI

Utafiti huu umechanganua taratibu za utohozi wa nomino za Kikamba kutoka Kiswahili kwa madhumuni ya kuainisha kanuni zinazohusika. Uchanganuzi umeongozwa na mtazamo wa Fonolojia ya vipande sauti huru ambao ni mojawapo ya mitazamo ya Fonolojia Zalishi. Kulingana na mtazamo huu, fonolojia ni mfumo sauti wenye rusu nne: rusu msingi, rusu fonimu, rusu silabi na rusu toni. Nadharia ya Mawimbi pia ilitumiwa kueleza sababu zilizochangia ukopaji katika lugha ya Kikamba. Utafiti wetu umeainisha nomino za Kikamba zilizokopwa kutoka Kiswahili, ukabainisha vigezo vya kifonolojia vilivyotumika na kuchanganua taratibu na kanuni za kifonolojia zilizofuatwa katika ukopaji huo. Vigezo vya fonolojia ya Kikamba ambavyo ni fonimu, silabi na sifa arudhi vimebainishwa. Pia, sababu zilizochangia ukopaji katika lugha ya Kikamba zimeelezwa. Data msingi ya utafiti ilikusanywa katika sehemu ya Kitui ya kati kupitia mbinu za mahojiano na uchunguzi wa kushiriki. Katika uwasilishaji, maelezo yameambatana na michoro na majedwali. Uchunguzi umedhihirisha kwamba katika kushughulikia maneno mkopo, mbinu tatu huhusika nazo ni: uchopekaji, udondoshaji na ugeuzaji maumbo. Utafiti wetu una nafasi ya kuchangia uwanja wa isimu lugha ya Kiafrika kwa jumla tukizingatia kwamba utohozi unaweza kutumika katika kulinganisha mifano ya fonolojia. Pamoja na haya, data ya matokeo ya uchunguzi wetu inaweza kuwasaidia wasomi wa isimu za lugha za Kiafrika. Vile vile, matokeo ya utafiti huu yanachangia kukua kwa lugha ya Kikamba kwani uchunguzi ulishughulikia mabadiliko yaliyofanyiwa maneno yaliyokopwa na hii ni njia moja ambayo lugha hutumia kukuza msamiati wake.

YALIYOMO

UNGAMO ii

TABARUKU iii

SHUKRANI iv

IKISIRI v

YALIYOMO vi

ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA x

SURA YA KWANZA 1

1.1 UTANGULIZI 1

1.2 Lugha Zinazoshughulikiwa 2

1.2.1 Lugha ya Kikamba 2

1.2.2 Lugha ya Kiswahili 4

1.3 Swala la Utafiti 6

1.4 Malengo ya Utafiti 7

1.5 Haipothesia 8

1.6 Sababu za kuchagua Mada 8

1.7 Upeo na mipaka ya utafiti 10

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada 12

1.8.1 Maandishi ya Kijumla ya Manenomkopo 12

1.8.2 Tafiti bayana kuhusu Utohozi Mkopo 14

1.8.3 Maandishi kuhusu ukopaji katika Kikamba 17

1.9 Msingi wa Kinadharia 18

1.10 Mbinu za utafiti 24

1.11 Kutambua manenomkopo 25

1.12 Kuchanganua data 26

1.13 Kuwasilisha data 26

SURA YA PILI 27

SABABU ZA KIISIMU JAMII ZILIZOCHANGIA UKOPAJI WA MANENO KATIKA KIKAMBA 27

2.1 Utangulizi 27

2.2 Kuiga mitindo ya lugha yenye hadhi ya juu 28

2.3 Athari za kiutamaduni katika maingiliano 30

2.4 Mwingiliano katika mazingira ya uwili lugha na wingi lugha usiodhabiti 33

2.5 Dini 34

2.6 Nia ya kuziba pengo katika lugha 35

2.7 Ndoa mseto 36

2.8 Hitimisho 37

SURA YA TATU 38

VIGEZO VYA FONOLOJIA YA KIKAMBA 38

3.1 Utangulizi 38

3.2 Fonimu za Kikamba 38

3.2.1 Konsonanti za Kikamba 39

3.2.2 Vokali za Kikamba 43

3.2.3 Mahali na kutamkia vokali za Kikamba kutegemea mwinuko na mlalo wa ulimi 44

3.3 Silabi za Kikamba 45

3.3.1 Muundo wa silabi za Kikamba 46

3.4 Sifa arudhi katika Kikamba 50

3.4.1 Shada katika Kikamba 50

3.5 Uwiano wa vipengele vya kifonolojia 51

3.5.1 Vibadala vya Irabu 52

3.5.2 Irabu za wakaa mrefu 53

3.6 Vibadala vya konsonanti 55
3.6.1 Vipasuo 55
3.6.2 Vikwamizwa 56
3.6.3 Vizuiwa-kwamizwa 57
3.6.4 Nazali 58
3.6.5 Kitambaza 59
3.7 Vibadala vya silabi 60
3.8 Hitimisho 63
SURA YA NNE 65
TARATIBU ZA UTOHOZI FONOLOJIA 65
4.1 Utangulizi 65
4.2 Utohozi fonimu 65
4.2.1 Utohozi vokali 66
4.2.2 Utohozi wa Konsonanti 68
4.3 Utohozi Silabi 80
4.4 Utohozi arudhi 82
4.5 Hitimisho 83
SURA YA TANO 87
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO 87
5.1 Utangulizi 87
5.2 Muhtasari 87
5.3 Matokeo ya utafiti 88
5.4 Mahitimisho 91
5.5 Mapendekezo 92
MAREJELEO 95
KIAMBATANISHO 100
MANENOMKOPO YA KIKAMBA KUTOKA KISWAHILI 100

ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA

CH - Toni Chini

FA - Fonolojia Arudhi

FL - Fonolojia Leksishi

FM - Fonolojia Mizanishi

FZ - Fonolojia Zalishi

FZM - Fonolojia Zalishi Mageuzi

JU - Toni Juu

I - Irabu

K - Konsonanti

KI - Konsonanti - Irabu

K-V - Konsonanti – Vokali

SZ - Sarufi Zalishi

V - Vokali

X - Pigo Shada

σ - Silabi

$ - Mpaka wa Silabi

/ / - Uwasilishaji wa Fonimu

[ ] - Unukuzi Fonetiki

> - Mwelekeo wa mabadiliko kwa maana ya “hutamkwa kama” au “hugeuka kuwa”

SURA YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI

Utafiti huu unaangazia fonolojia ya nomino za Kikamba zilizokopwa kutoka Kiswahili kwa kubainisha kanuni za kiisimu zinazohusika. Kila lugha inadhihirisha kiwango fulani cha ukopaji wa maneno na kwa hivyo maneno mkopo ni tukio muhimu katika isimu. Lugha mbili au zaidi zinapotagusana zinaathiriana. Lugha yenye hadhi ya juu ndiyo huwa na athari katika lugha ya hadhi ya chini. Utafiti huu unajikita katika ukopaji wa hadhi (Bynon, 1977 na Verma na Krishnaswanny, 1989). Ukopaji husababisha matokeo mbalimbali. Baadhi ya matokeo hayo ni pamoja na uwili lugha na utohozi miongoni mwa mengine.

Ukopaji ni hali ya kuhamisha umbo au maana kutoka lugha moja hadi nyingine kwa sababu mbalimbali kama vile kukosa msamiati wa kutajia dhana au jambo fulani, sababu za kiteknolojia, utamaduni tofauti na kadhalika. Kukopa ni mbinu inayotumiwa na lugha zote ulimwenguni kurutubisha msamiati wake. Ukopaji unaweza kutokea katika viwango vyote vya lugha, yaani, sintaksia, semantiki, fonolojia, mofolojia au leksia. Kuna njia nyingi za kukopa dhana, kwa mfano kukopa sisisi, kukopa kwa tafsiri na utohozi. Kukopa sisisi ni kukopa moja kwa moja; yaani maneno yananukuliwa yalivyo na kutumiwa hivyo. Kukopa kwa tafsiri kunahitaji maneno kufasiriwa katika lugha kopaji. Utohozi unahusu kubadilishwa kwa maneno yaliyokopwa kwa kuzingatia fonolojia, mofolojia na semantiki ya lugha pokezi. Uchunguzi huu umeegemea utohozi fonolojia ambao unazingatia utamkaji wa lugha pokezi.

1.2 Lugha Zinazoshughulikiwa

1.2.1 Lugha ya Kikamba

Kikamba ni lugha inayozungumzwa na watu waitwao Wakamba nchini Kenya. Mollig na Heinne (1980) wakimnukuu Guthrie (1948) waliainisha wazungumzaji wa kibantu katika makundi matano; Kikamba kikiwa miongoni mwa lugha za kibantu za tapo la kati. Lugha hii huwekwa katika kikundi kimoja na lugha ya Gikuyu, Kimeru, Kitharaka, Kiembu na Kimbeere.

Neno 'Kikamba' ambalo linarejelea lugha yenyewe limeundwa kwa mofu (ki) ambayo ni kiambishi na (-Kamba-) ambayo ni mzizi. Katika maandishi yanayohusu Kikamba, neno 'kamba' limetumiwa kwa maana ya watu na pia lugha. Tunasisitiza kwamba neno hili ni mzizi tu ambao unahitaji kupachikwa viambishi mwafaka kulingana na mukhtadha wa matumizi ili kuleta maana yake kisemantiki. Mzizi '-kamba-' unapowekwa kiambishi awali (u) na tamati (ni) tunapata neno "ukambani" kwa maana ya nchi ya asili ya wakamba. Pia mzizi huu ukiongezwa kiambishi awali (m) huunda neno "mkamba" kwa maana ya umoja wa wakamba. Inaaminika kwamba wakamba walitoka 'Kiima Kyeu (mlima mweupe) yaani Kilimanjaro na kuhamia sehemu ya Machakos iitwayo 'Ulu' au 'Kyulu' (Kioko, 2012).

Kulingana na historia, Wakamba walikuwa wawindaji hodari wa ndovu kwa minajili ya kupata pembe walizozibadili kwa shanga na nguo kutoka kwa Waarabu. Katika karne ya kumi na tisa, Wakamba walijishughulisha na misafara ya kibiashara kutoka bara hadi pwani. Katika miaka ya 1960, Wakamba walisaidia kusafirisha bidhaa kutoka Mombasa

hadi Lamu wakiwa pamoja na jamii ya Mijikenda. Hii ni njia mojawapo iliyopelekea kuhama kwa Wakamba wengi hadi katika sehemu kadhaa nchini Kenya na pia Tanzania. Pia Wakamba wanajulikana kwa usanii wao hasa katika kutengeneza vikapu na vifaa vya udongo (Kioko, 2012). Ingawa wakamba wako karibu na mji wa Nairobi kuliko Mombasa, utangamano wao hasa kiutamaduni unaegemea sana upande wa Pwani na wala sio Nairobi. Hii ndiyo hali inayodhihirika katika eneo la utafiti.

Jamii ya Wakamba hupatikana kwa wingi katika kaunti za Machakos, Kitui na Makueni (Joshua, 2013). Pia kuna Wakamba wanaoishi katika eneo la Mwea wilayani Kirinyaga, Ithanga katika wilaya ya Thika, Shimba Hills wilaya ya Kwale, Mariakani wilaya ya Kaloleni na pia katika kaunti ya Tharaka Nithi. Mto Athi huigawa ardhi inayomilikiwa na Wakamba katika sehemu mbili. Upande wa Magharibi na Mashariki mwa Mto Athi kuna kaunti za Makueni na Machakos. Kusini Mashariki kunayo kaunti ya Kitui. Mto Athi kwa hivyo unaashiria umuhimu wa kijiografia pamoja na kilahaja. Wakamba wamepakana na Wakikuyu, Wambeere, Waembu na Watharaka upande wa Magharibi.

Kulingana na hesabu ya idadi ya watu nchini Kenya ya 1989, wazungumzaji wa lugha ya Kikamba walikuwa zaidi ya milioni mbili unusu. Katika mwaka wa 1999 walifikia karibu milioni tatu. Kwa sasa idadi kamili ya wakamba ni takribani milioni nne (UNHCR, 2013). Miongoni mwa hawa karibu nusu yao ni wakazi wa kaunti ya Kitui.

Maundu (1980) aliziainisha lahaja za Kikamba katika aina nne, lahaja mbili zinazozungumzwa wilayani Kitui ambayo sasa ndiyo kaunti ya Kitui, mbili katika wilaya

ya Machakos. Chimbuko la lahaja hizi ni lahaja kuu mbili zinazotambulikana na Wakamba kuwa lahaja ya Kitui na lahaja ya Machakos. Kwa mujibu wa Mutiga (2002), lahaja za kĩmasaku na kĩkĩtui hutofautiana kupitia kwa toni katika maneno, sauti na leksia. Kwa mfano, pale lahaja ya kĩmasakũ inapotumia toni ya juu, kikitui mara nyingi hutumia toni ya chini. Kwa mujibu wa utafiti huu, lahaja ya kĩkĩtui ndiyo iliyoshughukiwa hasa ile ya Kitui ya kati.

1.2.2 Lugha ya Kiswahili

Kiswahili ni lugha ya Afrika Mashariki na kati iliyoenea na kujulikana na wengi zaidi katika eneo hili kuliko lugha nyingineyo ya Afrika (Ali, 2010). Ni lugha ya kibantu inayotumiwa kwa mawasiliano sehemu za Afrika ya kati na mashariki. Aidha, ni lugha ya taifa nchini Kenya, Tanzania na Uganda. Vile vile ni moja kati ya lugha nne za taifa nchini Congo (Mwita, 2009).

Watafiti kama vile Kishe (2002), Ruhumbika (2006), na Gromova (2008) hawajakubaliana kuhusu idadi ya lahaja za Kiswahili na mipaka yake, ambazo zinazungumzwa Pwani na Visiwani Unguja na Pemba. Hata hivyo, lahaja zifuatazo zimetajwa na wengi wao: Kiunguja, Kiamu, Kimvita, Kihadimu, Kitumbatu, Kipemba, Kimtang'ata, Kivumba, Chichifundi, Ki-siu, Ki-tikuu, Chi-miini na Kingwana. Kiswahili sanifu ni lahaja iliyosanifishwa kutokana na Kiunguja (Gromova, 2008). Hii, ndiyo lahaja rasmi inayofunzwa shuleni, inayotumiwa katika maandishi na katika utangazaji.

Idadi kubwa ya Waswahili hupatikana sehemu ya mwambao wa pwani ya Afrika mashariki ambapo wengi wao ni wafuasi wa dini ya Kiislamu (Mwita, 2009). Kwa kuwa

wamekuwa na dini hiyo kwa karne nyingi, maisha yao kwa jumla, ndoa, ushirikina na kadhalika yamefungamana sana na Uislamu hivi kwamba ni vigumu kuyatenganisha. Itikadi na desturi zote za Waswahili haziwezi kuzungumzwa kwa undani bila kugusia dini ya Kiislamu.

Msingi wa Kiswahili sanifu ni lahaja ya Kiunguja, lakini kwa vile Kiswahili sanifu ni lugha inayotumiwa na watu wengi wenye tofauti za kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa, imeathiriwa sana na msamiati kutoka lugha mbalimbali (Zawawi, 1979:36). Ni vigumu kuifahamu idadi kamili ya watu wanaozungumza Kiswahili. Lugha hii inatumika kama lugha ya kwanza na wakazi wa mwambao wa Afrika Mashariki kuanzia Somalia upande wa kaskazini hadi visiwa vya Komoro upande wa kusini (Massamba, 1990).

Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kiafrika zilizoenea zaidi barani Afrika. Hatua ya kuchaguliwa kwa Kiswahili kuwa mojawapo wa lugha zinazotumika katika Muungano wa Nchi za Kiafrika kumeipa lugha hii hadhi kubwa. Lugha ya Kiswahili imekua na kuvuka mipaka. Haitumiki Afrika mashariki pekee bali ulimwenguni kote, hususan katika vyuo vikuu. Isitoshe, Kiswahili kinatumika katika matangazo kwenye idhaa mbalimbali ulimwenguni kwa mfano Marekani, Ujapani, Ufaransa, Uchina na Uingereza. Pia lugha ya Kiswahili ni lingua franka katika Afrika ambapo Kiswahili kinatumika kama lugha ya pili na mamilioni ya watu hasa nchini Kenya, Tanzania, Uganda na hata Zaire Mashariki. Vile vile, kunao wazungumzaji wa Kiswahili Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi na hata katika nchi za Uarabuni (Massamba, 1990).

1.3 Swala la Utafiti

Kazi hii inatoa uchanganuzi wa kiufafanuzi kuhusu fonolojia ya maneno mkopo. Utafiti wetu ulichunguza fonolojia ya nomino zilizokopwa kutoka lugha ya Kiswahili na kuingizwa katika lugha ya Kikamba cha Kitui ya kati.

Dhana ya utohozi mkopo ni maarufu katika Isimu kwa kuwa ni mojawapo ya mbinu za uundaji wa istilahi zinazorutubisha lugha. Kuna tofauti kubwa kati ya konsonanti za Kikamba na zile za Kiswahili. Pia miundo ya silabi katika lugha hizi mbili hutofautiana hasa pale ambapo Kiswahili kina silabi za konsonanti pekee ilhali Kikamba hakina. Uchunguzi huu ulifanywa kutokana na sababu kwamba licha ya hitilafu hizi, maneno ya mkopo kutoka Kiswahili yanadhihirika katika lahaja ya Kikamba inayozungumzwa katika Kitui ya kati. Usilimisho wa kifonolojia wa maneno mkopo ni jambo la lazima katika kila lugha. Hata hivyo, kila lugha inatumia utaratibu tofauti na hivyo ni muhimu kuchunguza mbinu zinazotumiwa na Kikamba katika kushughulikia hitilafu zilizoko baina ya vigezo vya kifonolojia vya Kikamba na vile vya Kiswahili. Taratibu hizi zimesababisha mabadiliko katika fonolojia ya Kikamba ambayo yanastahili kuchunguzwa.

Watafiti wa awali waliotalii lugha ya Kikamba wameshughulikia mada kama vile historia, utamaduni, lahaja tofauti na mada zingine. Vipengele vya fonimu, silabi na sifa arudhi havijashughulikiwa. Kwa hivyo utafiti haukuwa na budi kutekelezwa ili kuliziba pengo hili kupitia mbinu na misingi ya nadharia ya kisasa.

Katika lugha iliyotafitiwa, kuna utajiri wa msamiati wa nomino unaodhaniwa umetokana na lugha ya Kiswahili. Ukopaji wa maneno hautokei tu bila utaratibu wowote. Kuna njia mbalimbali zinazohusika katika uhamishaji wa maneno na tulichunguza namna maneno yanavyohamishwa kutoka lugha kopezi (Kiswahili) na kutiwa katika lugha pokezi (Kikamba). Utafiti huu ulijikita katika kiwango cha fonolojia ambapo maneno ya lugha kopezi hutoholewa ili yakubaliane na mfumo wa lugha pokezi.

Wazungumzaji wa lugha ya Kikamba hukabiliwa na tatizo la kuchopeka vokali au konsonanti mahali zisipohitajika wanapotamka baadhi ya maneno ya Kiswahili, kwa mfano '*mukate*' badala ya 'mkate'. Pia Wakamba hudondoa konsonanti kama vile 'h' kutoka mahali pake, kwa mfano, '*saani*' badala ya 'sahani'. Kwa hivyo ilitokea haja ya kuchunguza fonolojia ya Kikamba ili kubaini sababu za matatizo haya hasa katika kutamka maneno ya Kiswahili yanayopatikana katika Kikamba.

1.4 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuthibitisha ya kwamba maneno ya mkopo yanadhihirika katika lahaja ya Kikamba ya Kitui ya kati. Maneno haya yanatokana na kutagusana kwa lahaja hii na lugha ya Kiswahili pamoja na lugha nyinginezo kama vile Kitharaka.

Uchunguzi huu ulitazamia kutimiza malengo mahususi yafuatayo:

1. Kubainisha sababu zilizochangia Kikamba kukopa nomino kutoka lugha ya Kiswahili.
2. Kubainisha vigezo vya kifonolojia vinavyohusika maneno yanapokopwa na kuingizwa katika Kikamba.

3. Kuchanganua taratibu na kanuni za kifonolojia za utohozi wa nomino katika lugha ya Kikamba.

1.5 Haipothesia

Utafiti huu ulizingatia tahadhania zifuatazo:

1. Nomino za Kikamba zilizokopwa kutoka Kiswahili zilitokana na sababu za kiisimu-jamii.
2. Utohozi wa nomino za Kikamba kutoka Kiswahili unazingatia vigezo vya fonimu, silabi na sifa arudhi.
3. Nomino mkopo za Kikamba kutoka Kiswahili zinabainisha taratibu za utohozi fonimu, utohozi silabi na utohozi arudhi.

1.6 Sababu za kuchagua Mada

Mtafiti wa kazi hii ni mzungumzaji asilia wa lugha ya Kikamba. Kuchagua lugha hii kunaoana na pendekezo la mwanaisimu Milroy (1987) anayesema kuwa umilisi wa lugha ya sehemu ya utafiti ni muhimu katika utafiti wa kiisimu.

Ukopaji wa maneno ni sehemu muhimu ya isimu na huongeza uelewa wetu wa uendelezaji wa mahusiano miongoni mwa lugha za ulimwengu. Utafiti huu utachangia tafiti zilizoko kuhusu ukopaji wa maneno na hasa kuonyesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyoathiri lugha zingine nchini Kenya (Mwita, 2009).

Mwanafunzi wa isimu na isimu jamii katika bara la Afrika na nchini Kenya kwa jumla analazimika kutumia data ambayo haihusiani na mazingara yake. Utafiti huu utachangia

data mwafaka ya kutumika inayojikita katika mazingira ya kiafrika na yanayohusu hali halisi ya mawasiliano katika nchi ya Kenya. Zaidi ya hayo, data hii itawezesha kuelewa mazingira ya kijamii na vipengele vya kiisimujamii katika bara la Afrika (Batibo,1995).

Tafiti za awali zinazohusu kuingiliana kwa lugha nchini Kenya zinaegemea upande wa mijini ambapo dhana ya kuingiliana kwa lugha kijiografia haijitokezi. Utafiti wetu utachanganua matokeo ya kupambana kwa lugha katika mazingira ya mipakani na mashambani (Batibo,1995). Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu ukopaji (kwa mfano Mathooko 2004) zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, tafiti kupitia lugha ya Kiswahili zinahitajika.

Wanafunzi na wageni wanaojifunza lugha ya Kikamba wanaweza kutumia data ya manenomkopo kujifunza na hata kurekebisha makosa ya kifonolojia. Data ya manenomkopo inaweza kutumiwa kutafsiri lugha ya Kiswahili kwa Kikamba au Kikamba kwa Kiswahili. Uchunguzi huu una nafasi ya kuchangia usomi wa Kiswahili na isimu za lugha za kiafrika kwa jumla. Mifano ya manenomkopo inaweza kufaidi utafiti wa fonolojia hasa wa lugha za kibantu. Data ya maneno mkopo inaweza kutumiwa katika isimu linganishi hasa fonolojia ya lugha tofauti. Kazi hii inaweza kutoa utaratibu wa utohozi wa maneno mkopo (Kharusi, 2012).

Lugha ya Kikamba husawiri matumizi ya manenomkopo. Kama ilivyobainika hapo awali, mada hii itadhihirisha kuwa lugha ya Kikamba imekua kutokana na utohozi wa manenomkopo ya Kiswahili. Utafiti huu utasaidia kubainisha athari za lugha ya Kikamba

katika lugha ya Kiswahili. Athari hii inatokana na hali ya kutumia muundo wa Kikamba katika Kiswahili. Kazi hii itarejelewa na wasomi wa hapo baadaye hasa kuhusu mabadiliko yanayotokea katika utohozi wa maneno kutoka Kiswahili (Ngesu, 2004).

Nchini Kenya, Kiswahili ni somo la lazima katika viwango vya shule za sekondari na msingi Uchunguzi huu unaweza kutumiwa katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili shuleni kwa kuonyesha chanzo cha makosa ya kimatamshi. Utafiti huu utawasaidia wasomi wanaozungumza lugha ya Kikamba kuboresha matamshi yao kwani lugha ya kwanza inaathiri ujifunzaji wa lugha ya pili (Thuku, 2010).

Wasomi waliotafiti lugha ya Kikamba hawakushughulikia fonolojia ya manenomkopo, kuna haja ya uchunguzi kufanywa ili kutoa nuru kuhusu dhana hii kwa kubainisha aina ya ukopaji inayohusika. Mbinu ya utohozi ndiyo inaonekana kutumika sana kwa sababu ni ya haraka na rahisi kutokana na sababu kwamba watu hawana wakati wa kuvumbua istilahi kutajia dhana ngeni. Hivyo basi kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu utohozi wa maneno katika Kikamba ili kuangaza taratibu za kifonolojia zinazohusika kupitia nadharia ya kisasa (Kharusi, 2012).

1.7 Upeo na mipaka ya utafiti

Kama tulivyoona katika utangulizi wa sura hii, dhana ya ukopaji ni pana mno kwa kuwa inahusisha viwango vya kileksia, kifonolojia, kisintaksia na kimofolojia. Katika uchunguzi huu, kiwango cha kifonolojia ndicho kilishughulikiwa. Hata hivyo, viwango hivyo vingine vya ukopaji pia ni muhimu katika kazi hii. Hivi ni kusema kwamba

vilirejelewa kwa madhumuni ya kutoa mwanga zaidi wa maelezo lakini havikushughulikiwa moja kwa moja. Kwa kuzingatia misingi ya fonolojia ya vipande sauti huru, uchanganuzi ulirejelea viwango vitatu vya utohozi: Utohozi fonimu, utohozi silabi na utohozi arudhi.

Utohozi fonimu ni dhana inayorejelea mageuko ya sauti bayana. Utohozi fonimu unatokea tu pale ambapo sauti inatumika badala ya nyingine. Mageuko haya huhusisha zile fomimu zilizo na uhusiano ama wa jinsi ya kutamka au mahali pa kutamkia. Utohozi silabi unahusu kugeuka kwa maumbo ya silabi. Lugha ya Kikamba husawiri silabi wazi yenye umbo la Konsonanti-vokali na vokali. Kwa hivyo, lugha hii inapokumbana na umbo la silabi ya Kiswahili lenye konsonanti pekee huchopeka sauti ya vokali ili kuafiki muundo wa silabi yake. Utohozi arudhi hurejelea mageuko ya idadi ya maumbo ya silabi katika neno.

Hata ingawa lugha ya Kikamba inapakana na lugha tofauti na huenda imekopa kutoka lugha hizo, utafiti huu ulishughulikia lugha ya Kiswahili tu. Kiswahili kina lahaja zaidi ya kumi na nane (Gromova, 2008). Lahaja hizi ni nyingi kiasi kwamba ni vigumu kwetu sisi kushughulikia kila moja ya lahaja hizi. Utafiti wetu ulijikita katika lahaja ya Kiswahili sanifu. Hii ndiyo lahaja inayotumiwa na wengi katika mazungumzo na pia katika maandishi ikilinganishwa na lahaja zingine za Kiswahili.

Lugha ya Kikamba ina lahaja mbili kuu: Kikitui na Kimasaku. Lahaja hizi zina tofauti chache za kimatamshi. Lahaja ambayo ilitumiwa katika utafiti huu ni ya Kikitui.

Uchaguzi wa lahaja hii ulitegemea imani kwamba ujuzi wa mzungumzaji wa lahaja hii unahitajika katika uchunguzi wa aina hii (Chomsky na Halle, 1968). Uamuzi huu ulimwezesha mtafiti kuhusisha ujuzi wake wa lahaja ya Kikitui.

Kwa ajili ya nafasi na wakati, utafiti wetu haukugusia maeneo yote ya kaunti ya Kitui kunakozungumzwa lugha hii. Ni matumaini yetu kuwa eneo lililochaguliwa la wilaya ya Kitui ya kati ni kielelezo cha hali ilivyo.

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Uchunguzi wetu ulizingatia maandishi kuhusu ukopaji na utohozi wa maneno. Kuna aina mbili za tahakiki ya maandishi. Tahakiki za kijumla na zile bayana. Maandishi muhimu kwa utafiti huu yanahusu ukopaji lugha kwa jumla na hasa utohozi wa maneno. Tahakiki ya maandishi katika uchunguzi huu yamechanganuliwa kutegemea viwango viwili:

1. Maandishi ya kijumla kuhusu manenomkopo.
2. Maandishi bayana kuhusu utohozi.

1.8.1 Maandishi ya Kijumla ya Manenomkopo

Tahakiki za kijumla za manenomkopo zinahusu ukopaji bila kujikita katika lugha maalum. Maandishi ya kijumla kuhusu ukopaji yameangazia mambo matatu yanayohusu, leksia zinazokopwa, sababu za ukopaji, na matokeo ya kisarufi.

Wataalamu wengi (Mwita 2009, Whiteley 1967, Lyons 1968, Bynon 1977 na Mbaabu 1996), wanaeleza maneno mkopo kama uhamishaji wa leksia kutoka lugha moja hadi nyingine. Wataalamu hawa wameshughulikia aina za leksia zinazokopwa pamoja na sababu za ukopaji. Watafiti hawa wameafikiana kwamba lugha inaweza kukopa leksia zozote lakini zile zinazokopwa zaidi ni nomino. Maneno mengi yanayokopwa hutaja dhana ngeni kutoka utamaduni tofauti.

Waandishi waliotajwa hapo juu wameelezea mambo mawili yanayosababisha ukopaji: mahitaji ya lugha na hadhi. Kukopa hutokana na utamaduni tofauti. Ukopaji unaotokana na hadhi hutokea pale ambapo lugha hukopa leksia ambazo zinapatikana katika lugha hiyo. Hapa leksia asilia hutumika sambamba na manenomkopo. Ukopaji wa hadhi hutokana na sababu za kujitambulisha na kundi fulani.

Waandishi hao pia wamezungumzia matokeo ya ukopaji ambapo wameafikiana kwamba lugha inayokopa leksia hulazimika kuzitohoa kulingana na kanuni za fonolojia ya lugha husika. Utohozi unahusisha mageuko ya vipengele au vipashio vya sauti ya lugha kopeshi na kuingiza vile vya lugha kopaji. Pia lugha hukopa na kutohoa mofolojia na leksia (semantiki) za lugha nyingine.

Baadhi ya tafiti zilizofanywa zimeonyesha kwamba ukopaji unaweza kuleta mabadiliko muhimu katika fonolojia na sarufi ya lugha kopaji. Newmann (2000) anatoa mfano wa Kihausa ambacho hakikuwa na fonimu /h/ kabla ya maingiliano yake na Kiarabu. Mbeleni, sauti /h/ ilikuweko katika lugha hiyo lakini kama alofoni ya sauti /f/ ikitokea

kabla ya vokali za nyuma kwa mfano: dafu [dahu] ‘kupikwa’. Kutokana na athari za Kiarabu, fonimu /h/ ilianza kutumika kikamilifu kama konsonanti katika lugha ya Kihausa. Mfano huu ni muhimu kwani ulituongoza kutambua ni kwa kiwango gani ambapo fonolojia ya Kikamba imeathiriwa na ukopaji.

Ingawa maandishi haya yanazungumzia ukopaji, ni ya kijumla na hayajashughulikia lugha bayana. Vile vile kuna maswala mengi ambayo hayajashughulikiwa hasa kuhusu matokeo ya ukopaji. Maandishi haya yanaweza kurejelewa katika utafiti huu, lakini tafiti bayana kuhusu utohozi zinahitajika ili kuangaza zaidi kuhusu mada ya utohozi wa maneno.

1.8.2 Tafiti bayana kuhusu Utohozi Mkopo

Tafiti bayana ni zile zinazohusu utohozi wa maneno katika lugha maalum. Tafiti bainifu zilizorejelewa zaidi katika uchunguzi huu ni zile zinazohusu utohozi katika lugha za Kibantu, kwa mfano, Ngesu (2004). Watafiti wengine kama vile Ball (1971), Houpe (1978), Mwihaki (1998) na Mwita (2009) wameandika kazi zao katika lugha ya Kiingereza.

Ball (1971) amelinganisha sababu zinazochangia utohozi wa maneno kutoka Kiarabu na Kiingereza katika lugha ya Kiswahili. Ametoa sababu za kidini, elimu, nasaba na shughuli mbalimbali . Kazi hii imeangalia sababu za kijamii zinazosababisha utohozi wa maneno kutoka Kiingereza. Baadhi ya sababu hizo zinahusiana na asasi za kijamii kama dini na elimu. Dini huwa na nafasi muhimu katika jamii. Kabla ya Waarabu na wamishonari kuingia Afrika Mashariki, Kiswahili kilikuwa kikitumiwa hivyo

wakalazimika kukitumia. Kwa kuwa walikuwa na utamaduni tofauti, walikosa maneno mwafaka kutajia baadhi ya maneno na hivyo wakalazimika kuyatohoa kutoka lugha zao. Pia kuingiliana kwa wazungumzaji wa lugha mbalimbali huchangia kubadilika kimuundo na kimsamiati kwa lugha zinazohusika. Baadhi ya matamshi na msamiati huzuka ili kukidhi mahitaji ya mazingira haya mapya.

Houpe, (1978) alichunguza idadi au kiasi cha manenomkopo katika makala ya Kiswahili. Alichunguza mada mbalimbali na aina za maneno yaliyokopwa. Utafiti wake umezingatia matumizi ya maneno mkopo kwa kipindi cha miaka kumi na minne. Houpe pia ameshughulikia sababu zinazosababisha ukopaji. Ni jambo la kimsingi na la kawaida lugha kukopa maneno kutoka kwa nyingine. Kila lugha ni toleo la mabadiliko, inaendelea kubadilika mradi tu inaendelea kuzungumzwa. Pia, sayansi na teknolojia hubadilisha maisha ya watu na kuingiza mambo mapya yanayohitaji kupewa istilahi mpya. Kazi ya Houpe ilirejelewa ili kuelewa sababu za ukopaji na aina za maneno yanayokopwa.

Zawawi, (1994) amebainisha mageuko ya kimofolojia. Utafiti wake unahusu mabadiliko ya nomino kutoka lugha ambazo si za Kibantu zinapoingizwa kwa Kiswahili. Zawawi alijadili kuhusu maneno yaliyokopwa hasa kutoka Kiarabu na kuingizwa katika Kiswahili. Anaonyesha namna maneno hayo yanavyoathiri sarufi ya Kiswahili. Kauli anazozitoa Zawawi ni kwamba maneno yaliyokopwa huchukua muundo wa lugha pokezi. Kwa mfano, waqt-wakati, adhuhr-adhuhuri. Uchunguzi wake umebainisha makundi ya nomino katika Kiswahili. Utafiti huu ulirejelewa kwa maana unamulika utohozi.

Mwihaki (1998) amechunguza kanuni za fonolojia zinazoongoza utohozi wa maneno ya Gikuyu kutoka Kiingereza. Pia ameshughulika vigezo vya fonolojia ya Gikuyu. Katika uchunguzi wake, ametoa sababu zinazosababisha ukopaji. Amesema kwamba sababu zilizofanya lugha ya Gikuyu kukopa kutoka Kiingereza ni kwamba lugha hizi zimetagusana kwa muda wa zaidi ya karne moja. Sababu zingine ambazo amezungumzia ni kutokana na utamaduni na teknolojia mpya. Amesema kwamba lugha ya Kiingereza ina hadhi kubwa ikilinganishwa na Gikuyu kwa sababu imekuwa ikitumika kama lugha rasmi katika maswala ya elimu, sheria na hata serikalini kwa muda wa zaidi ya nusu karne. Jukumu hili lilisababisha ukopaji wa leksia na kwa sababu hiyo lugha ya Gikuyu inasawiri maneno mengi ya mkopo kutoka Kiingereza.

Mwihaki (ibid) pia amefafanua manenomkopo kama leksia ya dhana inayotokana na lugha nyingine. Maneno haya yanapoingizwa katika lugha nyingine hutoholewa kulingana na fonolojia ya lugha inayokopa. Utohozi huhusisha kubadilishwa kwa vipashio vya lugha kopeshi na vile vipashio vya lugha inayokopa. Mwandishi huyu anaendelea kusema kwamba utohozi hauhusu tu fonimu bali huhusu vipashio vingine vikubwa vya kifonolojia kama vile silabi na sifa arudhi, kwa hivyo kazi hii ilikuwa ya manufaa zaidi katika uchunguzi huu kwa sababu imeangazia utohozi wa maneno katika lugha ya Kibantu. Misingi ya nadharia ilifuma mitazamo miwili: Fonolojia Tengenishi na Fonolojia Mizanishi. Nadharia hii inaweza kutumiwa katika utohozi wa Kikamba. Kazi hii pia imeweka msingi katika uchunguzi huu. Kwa hivyo utafiti huu wa Mwihaki unafaa kurejelewa katika utafiti unaohusu utohozi wa maneno katika Kikamba.

Mwita (2009) ameshughulikia usilimisho wa maneno mkopo ya Kiswahili kutoka Kiarabu. Kazi ya Mwita inaeleza jinsi maneno ya Kiarabu yanavyoingizwa katika Kiswahili na mabadiliko yanayofanyiwa fonimu za Kiarabu ili kutosheleza muundo wa lugha pokezi ambayo ni Kiswahili. Mwita anatambua kwamba maneno mkopo katika Kiswahili yamepanua miundo ya silabi za Kiswahili. Kiswahili na Kikamba ni lugha nasaba kwani zote ni za Kibantu na hivyo utafiti wa Mwita ulitufaa katika utafiti wetu hasa katika kubainisha mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea maneno yanapoingizwa katika lugha ya Kikamba kutoka Kiswahili.

1.8.3 Maandishi kuhusu ukopaji katika Kikamba

Kazi ya awali ya Johnson (1919) inatupa mwanga wa kulinganisha lugha ya Kikamba na ile ya Kiswahili. Katika kazi hiyo, mwandishi anabainisha upekee wa lugha za kibantu. Anaeleza kwamba lugha hizi zina uhusiano wa karibu unaodhihirisha mlingano wa kifonolojia, kileksika, kisintaksia na kimofolojia. Hali hii inarahisisha ukopaji wa maneno baina ya lugha hizi. Kazi ya Johnson ilirejelewa katika utafiti wetu kwani Kikamba na Kiswahili ni lugha za kibantu.

Ukopaji wa maneno umemulikwa katika kazi ya Whiteley (1963). Mwandishi huyu anachanganua maneno yaliyokopwa kutoka Kiswahili na Kiingereza na kutiwa katika lugha ya Kikamba. Kwa kiasi, anaelezea sababu za kiutamaduni ambazo zilitatiza maneno haya kujikita vilivyo katika mfumo wa Kikamba. Hata kama kazi hii inafafanua lahaja ya Machakos, ni kielezo kwamba lugha hukopa msamiati inapopambana na nyingine. Utafiti wetu ulipiga hatua mbele kwa kuonyesha sababu za kiisimu jamii zinazochangia ukopaji huu na namna maneno haya yanavyoingizwa katika lugha pokezi.

Utafiti unaohusu lahaja za Kikamba unatusaidia kuonyesha tofauti za viwango mbalimbali katika lahaja ya Kikitui. Kazi ya Kitavi (1992) inachangia katika utafiti huu. Kitavi amelinganisha lahaja ya Kitui kaskazini (lahaja ya Mwingi) na lahaja ya Machakos. Anatilia mkazo kwamba kila lugha ni tokeo la mabadiliko na itaendelea kubadilika mradi inazungumzwa. Anatoa ithibati kuhusiana na madai haya kwa kuonyesha sauti katika lahaja ya kaskazini mwa Kitui ambazo zinatofautiana na zila za lahaja ya Machakos. Utafiti wetu ulifaidi kutokana na maandishi haya kwani lahaja ya Mwingi ina uhusiano na lahaja inayotumiwa katika Kitui ya Kati kwa kiwango fulani.

Mutisya, (1986) anabainisha upatanifu ulioko kati ya Kiswahili na Kikamba. Kuweko kwa upatanifu kati ya Kikamba na Kiswahili kunawezesha maneno kukopwa kwa urahisi na kuhamishwa kwa kubadilisha tu vipengele vichache. Kazi ya Mutisya ilitusaidia kulinganisha Kiswahili na lahaja ya Kikitui.

Ngesu, (2004) ameshughulikia usilimisho wa maneno mkopo ya lahaja ya Mwingi. Anaeleza sababu za kiisimu jamii zilizochangia ukopaji wa maneno katika lahaja ya Kikamba ya Mwingi. Kazi hii inatusaidia kutambua maneno mkopo katika lahaja ya Kikitui na kuonyesha mabadiliko ya kifonetiki yaliyotokea baada ya maneno hayo kutoholewa kutoka Kiswahili.

1.9 Msingi wa Kinadharia

Taaluma ya isimu na pia isimujamii imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali kila mmoja wao akichukua kipengele fulani cha lugha. Wote hawa wametumia msingi wa

nadharia fulani kuwaongoza katika kazi zao. Misingi ya nadharia ya kisasa inahitajika ili utafiti katika Kikamba ufanywe kwa njia bora zaidi na ya kisasa. Nadharia zilizorejelewa katika utafiti huu ni mbili: Nadharia ya Fonolojia zalishi (FZ) na nadharia ya mawimbi.

Fonolojia zalishi ni kitengo cha sarufi zalishi (SZ) inayotazama lugha sawa na mfumo wa ujuzi lugha unaojisawiri ubongoni mwa msemaji (Chomsky na Halle, 1968, na Goldsmith, 1990). Fonolojia zalishi hata hivyo imepitia mitazamo mingi sambamba na mpito wa kihistoria. Mitazamo hiyo ni Fonolojia Mageuzi, Fonolojia Leksishi, Fonolojia Mizanishi na Fonolojia vipande sauti huru. Ingawa mitazamo yote haikuhusishwa katika kazi hii, kwa minajili ya watafiti wa baadaye, ni muhimu kuifafanua kwa ufupi.

Fonolojia Mageuzi (FZM) ni mtazamo wa awali unaozingatia viwango viwili vya muundo wa sauti pamoja na sheria zinazofuma viwango hivi. Viwango vya sauti vinavyohusishwa katika nadharia hii ni kiwango cha fonetiki. Fonetiki hutumiwa kuwakilisha sauti zenyewe. Kiwango fonetiki huwakilisha sifa za sauti zinazohusika. Baadaye nadharia hii ilisemekana kuwa na udhahania kwa sababu ilizingatia fonimu na sifa zake huku ikipuuza vipashio vya Kifonolojia kama vile silabi na sifa arudhi. Udhahania huu ulipelekea kuibuliwa kwa nadharia zingine, mojawapo ikiwa Fonolojia Leksishi.

Fonolojia Leksishi ni mojawapo ya mitazamo ambayo ilichipuka kupunguza ufonimu wa Fonolojia Mageuzi. Mtazamo huu unazingatia viwango viwili vya sheria ambavyo ni sheria kirai na sheria leksia. Sheria hizi hushirikiana na mfumo wa kanuni sita ambazo ni:

Kanuni ngazi, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya kufuta mabano, kanuni ya kwingineko, kanuni ya ufinyu wa sifa na kanuni ya kuhifadhi muundo. Kanuni na sheria husawiri uwiano baina ya fonolojia na mofolojia. Nadharia hii haikutumiwa katika uchunguzi kwa sababu inazingatia zaidi taratibu za mofolojia.

Fonolojia Mizanishi (FZ) inajikita katika kuchunguza na kuwakilisha mifumo ya shada na wizani katika lugha. Shada huwakilishwa katika viwango vya silabi na neno kupitia matawi wizani au solo wizani. Uwakilishi huu unaashiria kwamba vipashio viwili, silabi na neno, ndivyo husisitizwa. Mtazamo huu haukutumiwa kwa sababu uchunguzi hauna vifaa vya kushughulikia fonimu na toni. Hata hivyo unaweza kuhusika panapozungumziwa shada. Nadharia iliyohusishwa kwa wingi ni ya Fonolojia ya vipande sauti huru.

Mbinu za uchanganuzi na uwasilishi data zilizingatia misingi ya Fonolojia ya vipande sauti huru iliyoasisiwa na Goldsmith. Nadharia hii inadai kwamba uwasilishaji wa kifonolojia huwa na vipashio au vipande mbalimbali vilivyo huru kama vile mkazo, toni, vokali na konsonanti. Vipashio hivi vyote hutokea katika viwango vilivyo huru. Fonolojia ya vipande sauti huru inategemea mpangilio wa kifonolojia unaofuma fonimu, silabi na toni. Uchunguzi unanuia kudhihirisha jinsi nadharia hii inavyotumika kusawiri taratibu za utohozi wa manenomkopo. Vilevile, uchunguzi wetu unakusudia kufafanua waziwazi na kuonyesha kuwa utohozi fonolojia huongozwa na kanuni na vigezo vya lugha husika. Uchunguzi wetu kwa hivyo ni mtazamo wa kisasa unaochunguza mfumo wa sauti kwa ukamilifu zaidi.

Kwa mujibu wa Goldsmith (1990), Fonolojia ya vipande sauti huru hufafanua mfumo wa sauti katika rusu. Mkabala wa nadharia hii hueleza rusu kama ngazi vipande huru vya kifonolojia vinavyohusiana na kujengana. Vipande hivyo vinaweza kuangaliwa pekee bila kuhusishwa na kingine. Mpangilio wa vipande huru unategemea rusu tatu: rusu fonimu, silabi na toni. Kila moja ya rusu hizi ina uhusiano wa moja kwa moja na rusu mgongo. Rusu mgongo ni ngazi msingi ambayo huambatanisha vitengo vya konsonanti na vokali. Hali hii inatokana na bia ya fonolojia na kwamba zina ulinganifu wa kimuundo. Lugha zote zinajumuisha sauti za konsonanti (k) na sauti za vokali (v).

Fonimu ni kipashio kidogo kabisa kilicho na uamilifu wa kutofautisha maana za maneno katika lugha. Sifa za uhusiano huo zinasawirika wazi katika jedwali tenganishi la rusu mgongo na rusu fonimu. Jedwali linafuma rusu hizo katika neno na kuonyesha uhusiano wa rusu hizo kupitia vistari vinavyounganisha vipengele hivyo. Tazama kielelezo kifuatacho katika neno /elɛvɛ/ (debe).

Kielelezo cha rusu fonimu.

Rusu mgongo	V	K	V	K	V
Rusu fonimu	e	l	ɛ	v	ɛ

Silabi (σ) ni kipashio kinachotumika kuelezea ruwaza za mwambatano wa fonimu wa lugha fulani. Mambo ya silabi katika neno moja hutenganishwa kwa mipaka – silabi ($)

Kielelezo cha jedwali kifuatacho kinadhihirisha muundo wa silabi wazi kwa kurejelea neno /ekɔti/ (koti) e $ kɔ $ ti: v $ kv $ kv



Toni ni ruwaza za kidatu katika kiwango cha neno. Kielelezo kifuatacho kinabainisha rusu toni kwa kurejelea neno [*ita*], neno [ita] likiwa na ruwaza ya juu –chini lina maana ya kitenzi ‘nyonga’. Neno (*ita*) likiwa na kidatu cha chini –juu huleta maana ya ‘ezeka’.

Kielelezo cha rusu toni.



Mpangilio wa rusu unahusiana kwa vile unaongozwa na sheria na kanuni za fonolojia. Rusu hizo ndizo huongoza utohozi wa maneno. Fonolojia Zalishi inategemea imani kwamba lugha zote hutawaliwa na kanuni za kijumla. Kwa mfano, mifumo yote ya kifonolojia inajumuisha sauti za konsonanti na vokali.

Nadharia ya mawimbi pia ilitumiwa katika utafiti huu kufafanua sababu za ukopaji katika Kikamba. Johannes Schmidt (1872) ndiye mtaalamu wa kwanza kupendekeza Nadharia ya Mawimbi. Nadharia ya Mawimbi hueleza namna vipengele vya kiisimu vinavyovumbuliwa na kusambaa katika maeneo yaliyo karibu mithili ya mawimbi yasambaavyo majini hasa kutoka mahali palipotoswa jiwe. Dhana hii hutumika katika isimujamii na pia isimu Historia.

Katika isimu linganishi dhana hii huangaza uhusiano uliopo baina ya lugha "Uainishaji Kijeni" yaani uainishaji wa lugha kwa kuzingatia uhusiano wa kinasaba (lugha nasaba). Aghalabu lugha nasaba hufanana kimuundo kwa kiwango kikubwa kwa sababu chimbuko la lugha hizi ni moja. Kutokana na uhamiaji na kupambana na lugha zingine, lugha hizi hutofautiana lakini bado huwa na chembe ya kulandani. Kule kufanana kunachangia uwezekano wa kila moja kukopa maneno kwa urahisi hasa kwa kubadilisha tu vipengele vichache.

Kwa mujibu wa Bynon (1977), nadharia ya mawimbi inafafanua namna vipengele vya lugha vinavyoweza kusambaa. Anaeleza kwamba iwapo lugha mbili nasaba zina mwingiliano wa kijiografia, kisiasa na kiutawala, kunaweza kuwa na udondoshi wa baadhi ya vizingasifa vya ndani. Katika kudondoshwa kwa vizingasifa, vinginevyo huundwa kwa minajili ya kutumika katika eneo linalozungumzwa lugha hizi mbili.

Lugha ambazo zilikuwa tofauti sana, sasa huwa zinafanana kwa kiasi kikubwa. Aidha, Bynon anatilia mkazo kwamba msambao wa vipengele vya lugha si lazima udhihirike baina ya lugha katika vikundi vyovyote vile mradi tu kuna mwingiliano wa aina fulani. Lehman(1962) anasisitiza kwamba nadharia ya mawimbi inachangia kueleza uhusiano uliopo katika lugha pamoja na kuchanganua mabadiliko yanayotokea katika lugha.

1.10 Mbinu za utafiti

Utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani. Maktabani, mtafiti alihusisha tahakiki ya vitabu mbalimbali, tasnifu, machapisho ya makala mbalimbali, majarida na kadhalika. Mtafiti alilazimika kusoma kazi na makala mbalimbali yaliyohusiana na kazi kwa lengo la kuweza kuifahamu vyema zaidi. Utafiti wa maktabani ulitumiwa kudhihirisha jinsi ambavyo utohozi hutekelezwa na pia kuonyesha misingi ya nadharia iliyohusika. Utafiti wa nyanjani ulitumiwa kukusanya data kwa njia mbili; mahojiano na uchunguzi wa kushiriki.

Mahojiano

Mbinu hii ilitumiwa kuwahoji wazungumzaji wa lugha ya Kikamba. Wazungumzaji hawa walitumiwa ili kupata uasilia wa utohozi. Mahojiano haya yalihitaji kudumishwa kwa mahusiano mazuri ili ukusanyaji wa data usikatizwe kwa njia yoyote (Mugenda, 1999). Tuliwahoji baadhi ya watu katika miktadha tofauti hususan dini, taaluma mbalimbali, elimu, uchumi, biashara, tamaduni na shughuli nyingine za kijamii. Tulitumia orodha ya maneno ambayo yalisomewa wahojiwa nao waliyatafsiri katika lahaja ya Kikamba cha Kitui ya Kati. Maneno haya yalikuwa katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili tusiathiri utamkaji wa wahojiwa.

Uchunguzi wa Kushiriki

Mbinu ya uchunguzi wa kushiriki ilitumiwa kwa maana matamshi yanahitaji mzungumzaji ambaye pia ni mwenyeji wa lugha husika. Kulingana na Chomsky na Halle, (1968) wasemaji wa lugha huwa na ufahamu wa kanuni zinazoongoza matumizi ya lugha hiyo. Mbinu ya ushiriki iliwezesha kukusanya leksia tofauti tofauti hasa kwa wale ambao hawajui kusoma na kuandika. Katika utafiti huu, tuliweza kushiriki katika mikusanyiko mbalimbali kama vile makanisani, sokoni, nyumbani, hospitalini na kwenye magari ya usafiri. Tuliweza kusikiza wazungumzaji wa Kikamba katika mazungumzo yao ya kawaida. Data kutoka mazungumzo na mijadala ilinukuliwa katika maandishi ya kawaida na ya kifonetiki. Njia hii ni mwafaka kwani watu waliweza kueleweka katika matumizi ya lugha ya uhalisi usioingiliwa na kutoweza kuathiri matokeo ya utafiti. Pale ambapo wahojiwa walishindwa kutoa majibu yaliyo na uhakika, njia ya uchunguzi wa kushiriki ilifaa sana.

1.11 Kutambua manenomkopo

Manenomkopo ya Kikamba yalitambuliwa kwa kulinganisha muundo wa maana na maumbo ya maneno, na ule linganifu wa Kiswahili. Utambuaji wa manenomkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili si rahisi kwani lugha hizi zina muundo wa fonolojia unaokaribiana. Hata hivyo, tamaduni za awali za Waswahili na Wakamba ni tofauti. Kwa hivyo, leksia zinazohusu mavazi, taaluma mbalimbali, vyombo vya nyumbani, zana mbalimbali na vyakula mbalimbali ndizo zilitumiwa kutambua istilahi ngeni katika leksia ya Kikamba.

1.12 Kuchanganua data

Data zilizokusanywa zilijumuishwa na kuchanganuliwa kwa utaratibu. Sauti ziliainishwa ili kubainisha sauti zilizogeuka. Pia mageuko ya sauti yalichunguzwa na kuweka wazi vigezo na kanuni za kifonolojia zilizotumiwa. Uchanganuzi wa data ulitegemea uhusiano wa vigezo vya kifonolojia. Kila kigezo cha kifonolojia kilizingatiwa pamoja na uhusiano wa vigezo hivi. Mahusiano ya vigezo husika yalielezwa kutegemea kanuni za fonolojia ya Kikamba.

1.13 Kuwasilisha data

Matokeo ya uchunguzi yaliwasilishwa kwa maelezo na udhihirishaji. Maelezo yalifafanua vigezo vya kifonolojia kama vile fonimu, silabi na sifa arudhi katika lugha ya Kikamba. Ufafanuzi wa utohozi fonimu, utohozi silabi na utohozi arudhi ulitolewa mifano na vielelezo vinavyohitajika. Matokeo pia yalihusu udhihirishaji wa majedwali na michoro matawi. Ufafanuzi wote ulilenga matokeo na mahitimisho elekevu.

SURA YA PILI

SABABU ZA KIISIMU JAMII ZILIZOCHANGIA UKOPAJI WA MANENO KATIKA KIKAMBA

2.1 Utangulizi

Dhana ya ukopaji wa maneno ni tukio la kiisimu na vilivile kiisimujamii (Whiteley 1963:162). Mtafiti analazimika kuzingatia sababu za kiisimujamii zilizopelekea ukopaji wa maneno kutoka lugha moja hadi nyingine. Msingi wa kinadharia uliotueleza kutalii sababu zilizochangia ukopaji wa maneno umejikita katika nadharia ya Mawimbi. Nadharia hii hueleza namna vipengele vya kiisimu vinavyovumbuliwa na kusambaa. Dhana hii imeangaza uhusiano wa kinasaba ambao unajitokeza katika lugha ya Kikamba na ile ya Kiswahili. Nadharia ya Mawimbi inaangaza mwingiliano wa lugha mbili nasaba kijiografia, kisiasa na kiutawala.

Iribemwangi (2013) akimnukuu Langacker (1968) anasema kwamba hakuna lugha ambayo wazungumzaji wake wamewahi kuingiliana na lugha nyingine na wakakosa kukopa chochote kutoka kwa lugha ile. Hivi ni kumaanisha kwamba, ukopaji maneno unatokana na mtagusano wa lugha. Kulingana na Hoofer (2005), moja kati ya matokeo ya mwingiliano wa kijamii na mawasiliano ni kuwepo kwa maneno mkopo katika jamii husika.

Kiswahili na Kikamba ni lugha nasaba. Lugha nasaba hufanana kimuundo kwa kiwango kikubwa kwa kuwa hizi zina chimbuko moja. Kufanana huku huchangia uwezekano wa kukopa maneno kwa urahisi hasa kubadili tu vipengele vichache. Ukopaji wa maneno katika kupanua msamiati wa lugha ni tukio linalodhihirika katika lugha zote ulimwenguni. Namna jamii inavyokua na vitu vipya kuingizwa, linakuwa jambo la dharura kwa lugha hiyo kuendeleza msamiati wake ili kutimiza jukumu lake katika jamii (Njeru, 1990). Kwa msingi huu, utafiti wetu hauna budi kutalii mambo yaliyochangia kuweko kwa maneno mkopo katika lugha ya Kikamba.

2.2 Kuiga mitindo ya lugha yenye hadhi ya juu

Lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika katika mwambao wa pwani kwa karne nyingi pamoja na kuingiliana na lugha nyingi kama vile kiarabu, kijerumani, kilatini, kiingereza na kadhalika. Wafanyabiashara wa kigeni na wamishonari walipofika katika pwani ya Afrika mashariki, walihitaji lugha ya mawasiliano. Kwa kuwa tayari Kiswahili kilikuwa kimeendelea sana, waliipokea lugha hii bila pingamizi na ikawa lugha sambazi. Jinsi wageni hawa walivyozidi kupenya barani, vivyo hivyo Kiswahili kilizidi kuenea.

Hatua kama vile usanifishaji wa Kiswahili 1928, Kiswahili kufanywa lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Tanganyika 1962 na kuwa lugha ya taifa nchini Kenya 1969, iliipa lugha hii kipao mbele. Pia kuingiliana kwa Kiswahili na lugha kama vile Kiarabu, Kilatini, Kijerumani, Kiingereza na Kifaransa kulichangia utajiri mwingi wa msamiati katika Nyanja nyingi kama vile kisheria, kielimu, usafiri na kadhalika. Kwa jumla, lugha

ya Kiswahili ndiyo lugha ya Kibantu ambayo imekua na kuendelea sana. Kwa hivyo utajiri wa msamiati wake umewezesha lugha zingine hasa za Kibantu kukopa maneno kwani maneno haya tayari yamejikita katika fonolojia ya Kibantu kwa jumla.

Wataalamu wa kiisimujamii wamebainisha kwamba lugha yenye hadhi ya chini hukopa maneno kutoka kwa lugha iliyo na hadhi ya juu wakati lugha hizi zinapoingiliana. Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya na pia lugha sambazi katika mji wa Kitui. Kiulinganishi, lugha ya Kiswahili ina hadhi ya juu kuliko Kikamba. Katika kuingiliana kwa lugha hizi, lugha ya Kikamba imekopa msamiati mwingi kutoka kwa lugha ya Kiswahili. Wazungumzaji wa lugha yenye hadhi ya chini hutamani mitindo ya kisasa ili waonekane wastaarabu. Nia hii imechangia zaidi maneno mkopo katika Kikamba cha Kitui ya kati (Ngesu 2004).

Majina ya siku yana viwakilishi asilia katika lugha ya Kikamba kwa jumla lakini utafiti wetu ulitambua kwamba katika Kikamba cha Kitui ya kati, majina ya siku hutambulishwa kwa kuyatohoa yale ya Kiswahili.

Kiswahili		**Kikamba cha Kitui ya kati**
/ɟumatatu/	>	/juma:tato/
/ɟumannE/	>	/jumainE/
/ɟumatanɔ/	>	/juma:tanɔ/
/alhamisi/	>	/alamisi/

/iɟuma:/ > /juma:/

/ɟumamɔsi/ > /juma:mɔsi/

/ ɟumapili/ > /juma:÷ele/

2.3 Athari za kiutamaduni katika maingiliano

Uundaji wa msamiati mpya ni jambo ambalo limekuwa likifanyika wakati wote ambapo binadamu amekuwa akimiliki na kutumia lugha (Mdee, 1986). Ni kupitia kwa lugha ambapo mila na desturi za jamii hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Dhana na vitu mbalimbali huelezwa kwa maneno tofauti na wazungumzaji wa lugha tofauti. Wakati jamii tofauti zinapoingiliana kwa muda mrefu katika hali ya uwili utamaduni na hasa usio dhabiti, baadhi ya dhana huwa zaidi katika lugha moja kuliko nyingine. Mwingiliano huu huleta dhana mpya katika jamii hizi ambazo huhitaji kupewa msamiati wa kuziwakilisha katika lugha zao. Katika hali hii, maneno mkopo hayana budi kutokea kwa kuwa kila dhana mpya inahitaji kupewa kiwakilishi. Njia rahisi ya kuzipa dhana hizi mpya viwakilishi mara nyingi huwa ni kutumia tu maneno yaliyopo katika lugha kopezi. Athari za kiutamaduni kwa hivyo huchangia sana maneno mkopo ya kileksika.

Katika utafiti wetu, tulitambua kwamba tofauti za kitamaduni zilichangia sana ukopaji wa maneno katika Kiswahili hadi Kikamba. Kwa mfano, wakamba walijulikana kwa kutembea masafa marefu wakitumia punda kubebea bidhaa zao. Kwa hivyo, msamiati unaorejelea vifaa vya usafiri unapopatikana katika lugha ya Kikamba bila shaka ni thibitisho kwamba ukopaji ulihusika.

Kwa mfano:

Kiswahili		**Kikamba**
/gari/	>	/ŋgale/
/baiskEli/	>	/÷asikili/
/basi/	>	/mbasi/
/tairi/	>	/taili/
/barabara/	>	/÷ala÷ala/

Vilevile katika utamaduni wa wakamba, msamiati uliohusu elimu rasmi haukuwepo kwani wakamba walikuwa na aina yao spesheli ya elimu ambapo watoto walifunzwa imani na itikadi za jamii yao. Elimu ya wazungu ilipoletwa Afrika, Kiswahili kilikopa baadhi ya maneno na baadaye Kikamba kikakopa kutoka kwa Kiswahili. Maneno yafuatayo yanadhihirisha ukopaji wa msamiati wa kielimu katika lugha ya Kikamba kutoka Kiswahili.

Kiswahili		**Kikamba**
/mwalimu/	>	/mwalimo/
/chaki/	>	/sɔka:/
/skuli/	>	/sukulu/
/ubaɔ/	>	/o÷wao/
/kalamu/	>	/kalamo/

/ɔfisi/ > /o÷isi/

/mtihani/ > /motiane/

/sahihi/ > /sai:/

Kutokana na utamaduni mpya wa kielimu, lugha ya Kikamba ilikopa msamiati unaohusu taaluma mbalimbali. Taaluma hizi hazikuwepo katika utamaduni wa Wakamba na hivyo wakalazimika kutohoa maneno moja kwa moja. Mifano ifuatayo inathibitisha hayo.

Kiswahili		**Kikamba**
/rais/	>	/laisi/
/pɔlisi/	>	/÷ɔlisi/
/mabati/	>	/ma÷ati/
/fundi/	>	/÷undi/
/ʧerahani/	>	/ʧala:ni/
/randa/	>	/landa/
/msingi/	>	/mosiŋgi/
/ɟEla/	>	/jEla/
/bEndEra/	>	/ki÷EndEla/
/diriʃa/	>	/ndelesja/

Baadhi ya maneno haya yanadhihirisha utamaduni tofauti na ule wa kiafrika hivyo kupelekea watafiti kufikia uamuzi kwamba hata lugha ya Kiswahili ilikopa msamiati huu kutoka lugha nyingine kama vile Kiarabu na Kiingereza. Utafiti wetu ulishughulikia maneno mkopo hata yale ambayo mbeleni yalikopwa kutoka lugha nyingine, kupitia Kiswahili kisha Kikamba.

2.4 Mwingiliano katika mazingira ya uwili lugha na wingi lugha usiodhabiti

Kuingiliana kwa wazungumzaji wa lugha mbalimbali huchangia kubadilika kimuundo na kimsamiati kwa lugha zinazohusika. Baadhi ya matamshi na msamiati hubadilika au hata maneno mapya kuzuka ili kukidhi mahitaji ya mazingira haya mapya. Haiwezekani lugha mbili kuingiliana na lugha moja kukosa kuathiri ile nyingine (Zawawi, 1979).

Wakaazi wa mji wa Kitui wanatoka katika makabila mbalimbali kama vile Wasomali, Wakamba, Waswahili, Wameru, Wagikuyu na kadhalika. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ndiyo inayotumika katika mawasiliano kati ya watu wa makabila tofauti. Hali hii imechangia pakubwa ukopaji wa maneno baina ya lugha zinazohusika.

Wengi wa wakaazi wa eneo la Kitui ya kati hufanya kazi katika mji wa Mombasa. Kwa hivyo, kuna mwingiliano wa kila siku kati ya wakaazi wa Kitui ya kati na wale wa mji wa Mombasa. Katika utafiti wetu wa nyanjani, tuliweza kutambua kwamba licha ya wazungumzaji wa Kikamba katika Kitui ya kati kuwa karibu na jiji la Nairobi, kiutamaduni wameathiriwa sana na utamaduni wa Waswahili. Utajiri wa msamiati katika

lugha ya Kiswahili unawezesha lugha zinginezo hasa za kibantu kukopa maneno kwa kuwa maneno haya tayari yamejikita katika fonolojia ya kibantu kwa jumla.

2.5 Dini

Dini huwa na nafasi muhimu katika jamii. Lugha ya Kiswahili ilikuwa ikitumika kwa muda mrefu kabla ya Waarabu, Wamishonari na wakoloni kuingia Afrika mashariki. Hii ndio sababu waliitumia lugha hii bila pingamizi kama lugha ya biblia na islamu. Lugha ya Kiswahili pia ilitumika kama lugha sambazi katika biashara.

Kama tulivyodokeza awali, mji wa Kitui unajumuisha makabila tofauti. Dini za Kikristo na Kiislamu zina mashiko sana katika mji huu. Katika maingiliano ya kueneza injili ya Kikristo na Kiislamu, msamiati mwingi umeingizwa katika Kikamba.

Kwa mfano:

Dini ya Kikristo

Kiswahili		**Kikamba**
/ʃEtani/	>	/satani/
/ɟEsu/	>	/jEso/
/bibilia/	>	/mbi÷ilia/
/dini/	>	/ndene/
/zaburi/	>	/sa÷ule/

/sabatɔ / > /sa÷atɔ/

Dini ya Kiislamu

Kiswahili		**Kikamba**
/msikiti/	>	/mosikiti/
/maɟini/	>	/majini/
/kurani /	>	/kolani/

2.6 Nia ya kuziba pengo katika lugha

Lugha inaweza kukopa msamiati kwa kukosa msamiati mwafaka katika muktadha maalumu ambapo lugha kopaji haikuwa nao mwanzoni. Aidha, kutokana na maendeleo ya kisayansi na teknolojia, dhana mbalimbali zimebuniwa na vitu vingi vimeundwa ambavyo vinahitaji kupewa maneno ya kuviwakilisha. Iwapo hakuna kisawe cha dhana hiyo ngeni, lugha hulazimika kukopa maneno kwa kuyatohoa au kupitia kwa tafsiri mkopo. Maneno mkopo husilimishwa kupitia mifanyiko ya kifonolojia na kimofolojia ili yakubalike katika lugha pokezi. Wazungumzaji wa lugha pokezi huyachukua maneno mkopo kama msamiati asilia wa lugha hiyo.

Kwa mfano:

Kiswahili		**Kikamba**	
pasi	>	*vasi*	[÷asi]
simu	>	*simŭ*	[simo]

kura	>	*kula*	[kula]
bahaʃa	>	*vaasya*	[÷a:sja]
hesabu	>	*îsavu*	[esa÷u]

Kama ilivyotajwa awali, maneno mkopo mengine katika Kikamba yanayotokana na Kiswahili yameingizwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza kupitia kwa Kiswahili.

Kwa mfano:

Kiswahili		**Kikamba**	
ʃilingi	>	*silingi*	[siliŋgi]
rEdio	>	*letiŭ*	[lEtio]
supu	>	*suvu*	[su÷u]
kaptEni	>	*kavuteni*	[ka÷utEni]
baiskEli	>	*vasikili*	[÷asikili]

2.7 Ndoa mseto

Kama tulivyotaja hapo awali katika sura hii, wazungumzaji wa Kikamba katika eneo la Kitui ya kati wameishi pamoja na makabila tofauti na hutangamana kila siku mahospitalini, makanisani, sokoni, shuleni na kadhalika. Kulingana na Nzioki (1982), wanawake katika jamii ya wakamba ndio walioshughulika zaidi katika biashara baina yao na makabila jirani. Wanawake hawakuonekana kama maadui na kwa hivyo jambo hili likachangia ndoa mseto.

Katika eneo la utafiti, familia nyingi zina aila zao katika pande mbili. Kwa mfano, kunazo ndoa mseto kati ya Waswahili na Wakamba, Wagikuyu na Wakamba na kadhalika. Ndoa mseto hizi zimechangia matumizi ya Kiswahili katika kuwasiliana na hali kadhalika kuchangia maneno kukopwa na kuingizwa katika msamiati wa Kikamba.

2.8 Hitimisho

Kunazo sababu si haba za kiisimu jamii ambazo zimechangia kuwepo kwa maneno mkopo katika lugha ya Kikamba. Kama tulivyokwishaeleza katika sura hii, lugha yenye hadhi ya chini hukopa sana maneno kutoka kwa lugha iliyo na hadhi ya juu. Msamiati mwingi wa mkopo katika Kikamba umetokana na lugha ya Kiswahili iliyo na uamilifu wa lugha ya taifa nchini na pia lugha ya mawasiliano mjini Kitui (Lugha sambazi).

Hali kadhalika, ukopaji katika lugha ya Kikamba katika eneo la Kitui ya kati umetokana na mwingiliano wa Wakamba na makabila mengine ambapo lugha ya mawasiliano imekuwa Kiswahili. Ndoa mseto kwa mfano zimechangia ukopaji wa maneno katika jamii husika. Dini ya Kiislamu na ile ya Kikristo pia imeingiza msamiati mwingi wa Kiswahili katika lugha ya Kikamba.

SURA YA TATU

VIGEZO VYA FONOLOJIA YA KIKAMBA

3.1 Utangulizi

Kimsingi, utafiti huu unahusu fonolojia ya maneno mkopo inavyotegemea vigezo vinavyodhihirika katika mfumo wa Kikamba. Kwa hivyo kuna haja ya kushughulikia vigezo vya fonolojia hiyo ya Kikamba. Nadharia iliyotumiwa katika kuchagua vigezo hivyo ni ile ya Fonolojia ya vipande sauti huru.

Katika sura ya Kwanza, tuliona kwamba kwa mujibu wa Goldsmith (1990), Fonolojia ya vipande sauti huru hutazama fonolojia kama mfumo wa sauti wenye rusu nne; rusu msingi, rusu fonimu, rusu silabi na rusu toni. Rusu hizi huwakilisha vigezo vitatu vya fonolojia kwa jumla na hasa muundo wa Kikamba; fonimu, silabi na toni. Vigezo vya fonolojia ya Kikamba vilivyoshughulikiwa ni pamoja na fonimu, silabi na sifa arudhi.

3.2 Fonimu za Kikamba

Fonolojia zalishi inategemea imani kwamba lugha zote hutawaliwa na kanuni za kijumla. Mojawapo ya kanuni hizo inasema kwamba mifumo yote ya kifonolojia inajumuisha sauti za konsonanti na vokali. Lugha ya Kikamba kama zilivyo lugha zingine, ina fonimu za aina mbili nazo ni konsonanti na vokali.

3.2.1 Konsonanti za Kikamba

Konsonanti ni fonimu ambazo zinapotamkwa, mkondo hewa huzuiliwa kwa namna fulani na kwa kadiri tofauti (Schane 1973, Hyman 1975). Konsonanti za Kikamba ni 19 (Kitavi, 1992). Pamoja na hizi, Mathooko (2004) anatambua konsonanti nyingine mbili ambazo zinapatikana katika sehemu ya Kitui Magharibi ambazo ni [r] na [Φ]. Utafiti huu unajikita katika Kikamba kinachozungumzwa Kitui ya Kati na kwa hivyo konsonanti hizi mbili hazikushughulikiwa.

Konsonanti za Kikamba ni kama zifuatazo:-

t, k, mb, nd, ŋg , s, ÷, Θ, nz, nΘ, m, n, ɲ, ŋ, ʧ, ndʒ, l, w, j

Kama ilivyo katika uchanganuzi wa kifonolojia kwa jumla, konsonanti za Kikamba zinaweza kuainishwa kwa kuzingatia jinsi ya kutamka na pahala pa kutamkia. Kupitia taratibu hizi mbili, konsonanti za Kikamba zinaweza kuwasilishwa kupitia jedwali.

Jedwali 3.1: Mahali na jinsi ya kutamka konsonanti za Kikamba

MAHALI PA KUTAMKIA / NAMNA YA KUTAMKA	MIDOMONI	MENONI	UFIZI	KAAKAA GUMU	KAAKAA LAINI
VIPASUO			t		k
VIPASUO NAZALISHI-AWALI	mb		nd		ŋg
VIZUIWA				tʃ	
VIZUIWA NAZALISHI				ndʒ	
VIKWAMIZO	÷	Ɵ	s		
VIKWAMIZO NAZALISHI		nƟ	nz		
NASALI	m		n	ɲ	ŋ
VILAINISHO			l		
VIYEYUSHO	w			j	

(Kitavi, 1992; Mathooko, 2004)

Jedwali hili linawakilisha muhtasari ufuatao wa aina za konsonanti kulingana na sifa za mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka. Kwa kuzingatia mahali pa kutamkia, tunapata konsonanti zifuatazo.

(i) Konsonanti za midomoni /mb/, /÷/, /m/, /w/

(ii) Konsonanti za menoni /Ɵ/, /nƟ/

(iii) Konsonanti za ufizi /t/, /nd/, /s/, /nz/, /n/, /l/

(iv) Konsonanti za kaakaa gumu /ɲ/, /j/, /tʃ/, /ndʒ/

(v) Konsonanti za kaakaa laini /k/, /ŋg/, /ŋ/

Sifa kulingana na jinsi ya kutamka:

(i) Vipasuo /t/, /k/

(ii) Vipasuo nazalishi /mb/, /nd/, /ŋg/

(iii) Vizuiwa /tʃ/

(iv) Vizuiwa nazalishi / ndʒ/

(v) Vikwamizo /÷/, /Ɵ/, /s/

(vi) Vikwamizo nazalishi /nƟ/, /nz/

(vii) Nasali /m/, /n/, /ɲ/, /ŋ/

(viii) Vilainisho /l/

(ix) Viyeyusho /w/, /j/

Mohammed (2001), anaeleza kwamba kwa kawaida, konsonanti hutumika katika mazingira ya awali kama konsonanti sahili au kama konsonanti changamano. Katika Kikamba, konsonanti hutumika tu mwanzoni mwa silabi. Wald (1989) anatambua kwamba konsonanti nazalishi za Kibantu zinapaswa kuchukuliwa kama fonimu zinazojisimamia na wala sio mchanganyiko wa nazali na vipasuo. Kwa hivyo katika Kikamba, [mb], [nd], [ŋg], [ndʒ], [nƟ] na [nz] ni fonimu zinazojitegemea.

Katika Kikamba, konsonanti huungana na viyeyusho. Fromkin na Rodman (1988), wanaeleza kuwa viyeyusho ni sauti ambazo ni nusu irabu na ambazo hutofautiana na

irabu kwa kuwa haziundi kilele cha silabi hadi pale zinapowekewa irabu. Mifamo ifuatayo inaonyesha konsonanti zinazotamkwa pamoja na viyeyusho kama silabi moja:

/m/ + /w/ kama vile *mwana* [mwana] - mtoto

/k/ + /w/ kama vile *mukwa* [mokwa] - kamba

/Θ/ + /j/ kama vile *uthyu* [oΘjo] - uso

/ɸ/ + /w/ kama vile *vwana* [ɸwana] - bwana

/t/ + /w/ kama vile *mutwe* [motwE] - kichwa

/s/ +/j/ kama vile *syana* [sjana] - wana

/ɸ/ + /j/ kama vile *muvya* [moɸja] - mtama

/t/ + /j/ kama vile *mavityo* [maɸitjɔ] - makosa

Konsonanti za Kikamba zina maumbo mawili; sahili na changamano. Konsonanti sahili huwakilishwa kwa herufi moja katika tahajia na unukuzi wa kifonetiki inavyotumiwa katika fonimu kama /t/ na /s/ za maneno [*tata*] (baba) na [*susu*] (nyanya).

Kielelezo cha Konsonanti sahili

Rusu msingi	K	K	K	K
	|	|	|	|
Rusu fonimu	t	s	m	n

Konsonanti changamano huwakilisha mwambatano wa herufi za tahajia au mchanganyiko wa alama za kifonetiki kama ilivyo katika fonimu /mb/ au /mbw/ za maneno [*mbui*] (mbuzi) na [*mbwau*] (mbao).

Kielelezo cha konsonanti changamano

Rusu msingi	K	V	V
Rusu fonimu	mb	u	i

Ni muhimu kutambua kwamba konsonanti za Kikamba hushirikiana na vokali katika kutenda kazi.

3.2.2 Vokali za Kikamba

Vokali ni sauti ambazo wakati wa kutamkwa kwake ala za sauti huwa hazikaribiani kiasi cha kuweza kusababisha kutatizika kwa hewa kama ilivyo katika utamkaji wa konsonanti. Ndeti (1972) anaeleza kwamba Kikamba kina vokali saba nazo ni /a/, /E/, /e/ /i/, /ɔ/, /o/ na /u/ kama ilivyo katika kielelezo kifuatacho.

Utambulisho wa vokali za Kikamba

Fonimu	**Tahajia**	**Maneno**	**Tafsiri/maana**
a	a	/mata/	mate
E	e	/mokatE/	mkate
e	î	/ekɔti/	koti
i	i	/silingi/	shilingi
ɔ	o	/indɔ/	mifugo
o	ŭ	/simo/	simu
u	u	/otuko /	usiku

Vokali za Kikamba zimeweza kuainishwa kimsingi kwa kutumia taratibu za mwinuko na mlalo wa ulimi. Kulingana na mlalo wa ulimi, tunatambua vokali za mbele, katikati na za nyuma. Kutegemea mwinuko wa ulimi, tunapata vokali za juu, za kati-juu, kati-chini na za chini. Mchoro ufuatao unaonyesha vokali za Kikamba kutegemea mwinuko na mlalo wa ulimi.

3.2.3 Mahali na kutamkia vokali za Kikamba kutegemea mwinuko na mlalo wa ulimi



Kutokana na mchoro huu, tunaweza kupata jedwali lifuatalo.

Jedwali 3.2: Vokali za Kikamba kutegemea mwinuko na mlalo wa ulimi

	Mlalo wa ulimi		
Mwinuko wa ulimi	**Mbele**	**Katikati**	**Nyuma**
Juu	i		u
Kati-juu	e		o
Kati-chini	E		ɔ
Chini		a	

Mathooko (2004) anaonyesha kwamba Kikamba kina wakaa mrefu. Anatoa mfano wa maneno *uka* [oka] (njoo) na *ũũka* [o:ka] (pata wazimu) ambapo kurefushwa kwa vokali /o/ kunasababisha tofauti ya maana. Hata hivyo, utafiti ulitambua kwamba sauti /o/ katika neno /o:ka/ ni sauti mbili tofauti.

3.3 Silabi za Kikamba

Silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho kwa ukubwa kiko kati ya fonimu na neno; ni kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno. Silabi ni mwambatano wa fonimu ambazo hujumuisha sauti moja ya vokali au konsonanti inayotumika kama badili ya vokali (Schane 1973 na Hyman 1975). Silabi hata hivyo hudhihirisha maumbo tofauti kulingana na vikwazo katika mfumo wa lugha husika.

3.3.1 Muundo wa silabi za Kikamba

Silabi zote za Kikamba ni wazi na hakuna hata moja inayoishia kwa sauti ya konsonanti bali huishia kwa sauti ya vokali. Lugha ya Kikamba ina maumbo matatu ya silabi ambayo ni umbo la ‘KV’, ‘V’ pekee na ‘KKV’.

Silabi za vokali pekee katika Kikamba hupatikana popote katika neno kama inavyodhihirika katika maneno yafuatayo:

ukî [oke] (asali) – mwanzoni mwa neno

sua (jua) – mwishoni mwa neno.

Kwa hivyo vokali o na a ni mifano ya silabi zenye umbo la vokali pekee.

Kielelezo cha silabi ya umbo la vokali pekee.



o ke$



Umbo la ‘KV’ ndilo hupatikana kwa wingi katika maneno ya Kikamba. Silabi hizi hutumika katika mazingira yote ya kifonetiki; mwanzo, kati na tamati kama inavyodhihirika katika maneno yafuatayo:

(i) [*tata*] (baba)

(ii) [*Mukate*] (mkate)

Kielelezo cha silabi za umbo la ‘KV’

Kielelezo cha neno ‘*tata’*



Kielelezo cha neno /mokatE/



Katika kielelezo hiki cha neno '*tata'* (baba), silabi ya kwanza imeundwa kwa konsonanti [t] na irabu [a]. Muundo huu ndio unaodhihirika kwa wingi katika lugha ya Kikamba.

Kwa mfano:

Kikamba	**Tafsiri**
/÷E$÷a/	roho
/mo$ka/	mke
/si$mo/	simu

Utafiti wetu pia ulitambua kwamba silabi za Kikamba huweza kuwa na muundo wa KKV. Kwa mfano, mwanzoni mwa silabi ya kwanza ya neno *mwana* (mtoto) kuna sauti ya nazali [m] na kiyeyusho [w]. Katika kutamka, [mw] hutamkwa kama sauti moja na kwa hivyo ni sauti mwambatano. Kielelezo kifuatacho kinadhihirisha hayo:



Katika muundo huu, viyeyusho /w/ na /y/ huunganishwa na konsonanti nyingine kuunda sauti mwambatano.

Kwa mfano:

mŭkwayŭ, mbwaŭ, mwanya na ndilisya.

Kiswahili		**Kikamba**
/mbaɔ/	>	/mbwa$o/
/diriʃa/	>	/ndelesja/
/nafasi/	>	/mwaɲa/
/mkwaɬu/	>	/mukwajo/

Kielelezo cha neno /mbwao/ (mbao)



Kielelezo cha neno /ndelesja/ (dirisha)



3.4 Sifa arudhi katika Kikamba

Fonolojia arudhi ni dhana inayorejelea maumbo lugha na sifa ambazo huwekwa kwenye vipashio vikubwa zaidi kuliko fonimu (Hyman 1975, Crystal 1985, Couper-Kuhlen 1986). Uchunguzi huu umejikita katika sifa arudhi mbili; shada na wakaa.

3.4.1 Shada katika Kikamba

Shada ni mkazo unaowekwa kwenye silabi au neno. Lugha zote zinabainisha viwango viwili vya shada; shada silabi na shada neno. Kutegemea taratibu za uchanganuzi za fonolojia mizanishi, alama ya X inaonyesha shada silabi. Silabi yenye shada kuu zaidi

katika neno huongezewa X kuelekea juu. Tazama kielelezo kifuatacho kinachorejelea maneno /kesikɔ/ (kijiko) na /ke÷ule/ (kufuli).

Kielelezo cha uwakilishi wa shada neno.

Shada neno		X				X	
Shada silabi	X	X	X		X	X	X
Umbo neno	kî	si	ko		kî	vu	lî

Kuna aina mbili za shada neno; shada huru na shada tuli. Shada huru huwekwa kwenye silabi yoyote katika neno na kwa kawaida, hutofautisha maana za maneno. Shada tuli nayo huwekwa kwenye silabi maalum katika maneno na kwa kawaida huweza kutabiriwa mahali inapowekwa.

Kwa mujibu wa Barlow (1960), lugha za Kibantu hutumia shada tuli. Kwa hivyo, lugha ya Kikamba hutumia shada tuli ambayo inawekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho. Shada tuli huwa na dhima ya kifonetiki pekee na haitumiwi kutofautisha maana ya maneno. Sifa arudhi inayobainisha maana za maneno za lugha ya Kikamba ni toni. Sifa hii haijashughulikiwa katika uchunguzi huu kwani uchunguzi wenyewe umelinganisha Kikamba na Kiswahili na lugha ya Kiswahili haina sifa arudhi ya toni.

3.5 Uwiano wa vipengele vya kifonolojia

Kiswahili na Kikamba ni lugha za nasaba moja kwa kuwa zote ni lugha za Kibantu. Lugha nasaba hazina budi kuwa na ulinganifu fulani katika viwango vya muundo na maana. Aidha, kila mojawapo ya lugha hizi haina budi kuwa na sifa maalum zinazoitambulisha. Katika sehemu hii, tunazilinganisha lugha mbili tunazozishughulikia

ili kubainisha zinavyofanana au kutofautiana. Muundo wa fonolojia wa Kiswahili na Kikamba unahusisha fonolojia vipande na fonolojia arudhi.

3.5.1 Vibadala vya Irabu

Katika kushughulikia irabu, Mwanaisimu Daniel Jones alibuni mfumo wa irabu ambao aliuita Irabu Msingi, (Mgullu, 1999). Ingawa irabu hizi msingi hazihusishwi na lugha yoyote, hutumiwa wakati wa kuzipambanua irabu zilizo kwenye lugha mbalimbali. Irabu zilizo katika Kiswahili na Kikamba zinaoana kwa kiasi kikubwa na irabu msingi. Kwa mujibu wa Daniel Jones, irabu msingi ni nane; miongoni mwake, irabu saba zinadhihirika katika lugha ya Kikamba. Lugha ya Kiswahili nayo ina fonimu za irabu tano ambazo ni /a/, /E/, /i/, /ɔ/ na /u/.

Fonimu za Irabu za Kiswahili na mahali zinapotamkiwa.



Ulinganifu wa irabu za Kiswahili, Kikamba na IPA

Kiwakilishi cha IPA	Othografia ya Kiswahili	Mnukuu	Othografia ya Kikamba	Mnukuu
a	a	kama	a	kama (ng'ombe)
E	e	lEtE	e	EtE
e			î	ke:ma (mlima)
i	i	imba	i	ina
ɔ	o	mikɔnɔ	o	mɔkɔ
o			ũ	mondo (mtu)
u	u	kuʧakurɔ	u	ndu:

Kwa kuwa Kiswahili kina irabu tano tu, maneno mengine yanayokopwa kutoka lugha hii na kuingizwa katika Kikamba hulazimika kuchukua miundo tofauti ya kifonetiki. Kwa mfano:

Kiswahili **Kikamba**

/kalamu/ > /kalamo/

/suruali/ > /suluale/

/ukuta/ > /okota/

/kitamba:/ > /ketamba:/

3.5.2 Irabu za wakaa mrefu

Lugha za Kiswahili na Kikamba zinadhihirisha kuweko kwa irabu za wakaa mrefu. Aidha, irabu pekee ndizo huwa na wakaa mrefu wakati irabu moja inatokea mahali

pamoja kwa mfululizo. Kama ilivyotajwa hapo awali, tumebainisha kwamba irabu za wakaa mrefu katika Kiswahili na Kikamba huwasilisha fonimu kamili na huchangia kusawiri maana tofauti zitumiwapo.

Mifano katika lugha ya Kiswahili

			Maana
/a/	/a/	/dawa/	uganga
/aa/	/aː/	/dawaː/	duwaa/shangaa
/o/	/ɔ/	/kɔndɔ/	vita
/oo/	/ɔː/	/kɔndɔː/	aina ya mnyama

Mifano katika Kikamba

		Mnukuu	**Tafsiri**
/a/	/a/	/maka/	shtuka
/aa/	/aː/	/makaː/	makaa (kuni)
/a/	/a/	/nda/	tumbo
/aa/	/aː/	/ndaː/	chawa
/i/	/i/	/ngi/	nzi
/ii/	/iː/	/ngiː/	punje/mbegu
/o/	/ɔ/	/ngɔ/	chui

/oo/ /ɔ:/ /ngɔ:/ moyo

3.6 Vibadala vya konsonanti

Lugha zilizotafitiwa yaani Kikamba na Kiswahili zilidhihirisha tofauti kubwa kwa upande wa konsonanti. Utafiti wetu una mashiko zaidi katika sehemu hii kwa kuwa maneno yanayokopwa yanapaswa kufuata utaratibu wa kusilimishwa ili yakubalike katika lugha pokezi.

Lugha ya Kiswahili ina fonimu za konsonanti ishirini na nne nayo ya Kikamba inazo kumi na tisa. Katika lugha mbalimbali, konsonanti huainishwa kwa kuzingatia namna konsonanti hizo zinavyotamkwa, (Mgullu, 1999). Kigezo hiki kimetumiwa kuainisha konsonanti za lugha zilizofanyiwa utafiti.

3.6.1 Vipasuo

Vipasuo ni sauti ambazo hutamkwa mkondohewa unapofunguliwa kabisa katika sehemu yoyote ya bomba la sauti na kisha unapita ghafla na kwa mlipuko. Lugha mbili zilizofanyiwa utafiti; Kiswahili na Kikamba zina vibadala vya vipasuo kama inavyodhihirika katika mifano inayofuata.

Kiswahili			**Kikamba**	
/p/	/pEtE/	>	/mb/	/mbEtE/
	/paka/	>	/mbaka/	

/t/ /tairi/ > /t/ /taili/

/d/ /dawa/ > /nd/ /ndawa/

/dErEva/ > /ndElEva/

/k/ /kaburi/ > /k/ /kaɸule/

/g/ /gari/ > /ŋg/ /ngale/

/b/ /bakuli/ > /mb/ /mbakuli/

Vipasuo vifuatavyo katika Kiswahili vina vibadala vingine katika Kikamba ambavyo sio vipasuo.

	Kiswahili		**Kikamba**
/p/	/pasi/	>	÷ /÷asi/
/b/	/kibarua/	>	÷ /ke÷alua/

3.6.2 Vikwamizwa

Vikwamizwa ni sauti ambazo hutamkwa wakati ala za sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo. Vikwamizwa katika Kiswahili ni /f/, /v/, /Ɵ/, /ð/, /s/, /z/, /x/, /ʃ/, /h/ na /Φ/.

Katika Kikamba, vikwamizwa ni /÷/, /Π/, /s/ na /nz/.

Mifano

	Kiswahili		**Kikamba**
/f/	/faili/	>	÷ /÷aili/
/v/	/varanda/	>	÷ /÷alanda/
Δ	/dhahabu/	>	Π /Πa:÷u/
/s/	/sabatɔ/	>	/s/ /sa÷atɔ/
/z/	/zaburi/	>	/s/ /sa÷ule/
/s/	/shilingi/	>	/s/ /silingi/
/h/	/sahani/	>	/h/ - hudondoshwa /sa:ni/
/Φ/	/ghasia/	>	/k/ /kasia/

Vikwamizwa hivi katika Kiswahili na Kikamba vinaweza kutumika katika mazingira yoyote ya kifonetiki kama vile mwanzoni, katikati na hata katika silabi ya mwisho katika neno.

3.6.3 Vizuiwa-kwamizwa

Vizuiwa – kwamizwa ni sauti ambazo huhusisha kufungiwa kabisa kwa hewa na ala za sauti kisha kuachiliwa ipite ghafla kwa mlipuko lakini ala haziachani kabisa bali huacha

mwanya mdogo ambapo hewa huendelea kupita kwa shida hivi kwamba inasababisha mkwaruzo (Habwe J. na Karanja P. 2004). Lugha ya Kiswahili ina vizuiwa-kwamizwa viwili ambavyo vinaweza kutumika katika mazingira yoyote navyo ni /ɟ/ na /ʧ/. Katika Kikamba, Vizuiwa-kwamizwa pia ni viwili ; /tʃ/ ambacho hakibadiliki katika matamshi isipokuwa katika maandishi na /ndʒ/ ambacho hakina kibadala cha aina yoyote ya konsonanti katika Kiswahili.

Kiswahili		**Kikamba**
/ɟ/	>	/j/ (nusu irabu)
/ɟuma:tatu/	>	/juma:tatu/
/ʧama/	>	/ʧama/

3.6.4 Nazali

Nazali ni sauti ambazo zinapotamkwa, ala za kutamkia hukutanishwa halafu kaakaa laini pamoja na kidakatonge huziba njia ya kuingilia kwenye chemba cha kinywa hivi kwamba hewa nyingi hutokea puani (Waihiga na K. W. Wamitila, 2003). Nazali katika lugha zinazofanyiwa utafiti yaani, Kiswahili na Kikamba zinafanana. Nazali hizi ni /m/, /n/, /ɲ/ na /ɲ/ kama zinavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

	Kiswahili		**Kikamba**
/m/	/matE/	>	/mata/
/n/	/mwana/	>	/mwana/
/ɲ/	/ɲuni/	>	/ɲoŋi/

/ŋ/ /ŋɔmbE/ > /ŋɔmbE/

3.6.5 Kitambaza

Kitambaza ni moja kati ya sauti za likwidi ambazo hazitolewi kwa mkwamizo wa haja ila ala sogezi hutatiza hewa kwa namna maalum na hutamkwa huku hewa ikiendelea kupita. Kitambaza hutamkwa ncha ya ulimi ikiwa imekita katika ufizi huku hewa ikiruhusiwa kupita kando kando mwa ulimi.

Utafiti wetu ulidhihirisha kwamba lugha mbili zilizofanyiwa utafiti zinashabihiana kwa kuwa zina kitambaza kimoja tu ambacho ni /l/. Utafiti huu pia umebainisha kwamba hakuna kimadende katika othografia ya Kikamba cha Kitui ya kati. Kutokana na data tuliyokusanya, inabainika kwamba maneno mengi yanayotokana na Kiswahili hubadilishwa yanapoingizwa katika Kikamba na kuwekwa kitambaza badala ya kimadende. Aidha, maneno ya mkopo yaliyo na kitambaza hukubalika katika Kikamba pasipo mabadiliko yoyote kwa sababu sauti hii iko katika utaratibu wa lugha pokezi.

Kiswahili		**Kikamba**
/r/	>	/l/
/suruali/	>	/suluale/
/gari/	>	/ŋgale/
/l/	>	/l/
/kalamu/	>	/kalamo/

/bakuli/ > /mbakoli/

3.7 Vibadala vya silabi

Kamusi ya isimu na lugha (TUKI, 1981) inasema kuwa silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho kwa kawaida ni kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno. Silabi ni sehemu ya neno inayotamkika na aghalabu husikika kama sehemu tofauti na nyingine katika msingi wa neno.

Kiswahili kina muundo wazi wa silabi zake huishia kwa vokali isipokuwa katika maneno ya mkopo. Lugha ya Kiswahili ina miundo mitano ya silabi ambayo ni muundo wa irabu pekee, konsonanti na irabu, konsonanti pekee, konsonanti mbili na irabu na mwisho konsonanti tatu na irabu.

Silabi za muundo wa irabu pekee katika Kiswahili hupatikana popote katika neno kama vile mwanzoni, kati au hata mwishoni mwa neno. Kwa mfano: katika neno ‘anga’, silabi ya kwanza imeundwa kwa vokali pekee.

$a$nga$

Rusu Msingi V K K V



Muundo wa konsonanti na irabu ndio unaotumika kwa wingi katika Kiswahili kama ilivyo katika Kikamba.

Kwa mfano: kita$bu

bata$

Kielelezo



Tofauti kubwa kati ya silabi za Kiswahili na Kikamba ni kuwa Kiswahili kina silabi za konsonanti pekee, jambo ambalo haliko katika Kikamba. Muundo wa silabi za konsonanti pekee hutokea mwanzoni au katikati mwa neno ila tu katika maneno mkopo ambapo kuna uwezekano wa kutokea mwishoni mwa neno.

Kwa mfano: $m$ka$tE

$m$ka$te - mwanzoni mwa neno.

mazungum$zo – katikati mwa neno.



Kama ilivyo katika silabi za Kikamba, silabi za Kiswahili pia huwa na muundo wa konsonanti mbili na irabu. Silabi zenye umbo hili hutokea mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno.

Kwa mfano:

$u$nga$ - mwishoni mwa neno

mwalimu - mwanzoni mwa neno

kenge$le – katikati mwa neno

Kielelezo cha rusu silabi.





Aina nyingine ya silabi za Kiswahili ni muundo wa silabi za konsonanti tatu na irabu. Muundo huu haujitokezi kwa wingi katika Kiswahili. Hii ni tofauti nyingine inayopatikana baina ya silabi za Kikamba na zile za Kiswahili kwani umbo hili haliko katika Kikamba. Hata konsonanti zinapofuatana tatu katika Kikamba, mbili huwa ni fonimu moja.

Mfano:

Chungwa chungwa (Kiswahili)

$mbwa$u (mbao) - Kikamba

3.8 Hitimisho

Sura hii imebainisha vigezo vya fonolojia ya Kikamba. Imebainika kwamba Kikamba kina vigezo vya fonimu, silabi na sifa arudhi. Uchunguzi umetambua vokali saba na konsonanti kumi na tisa za Kikamba. Kwa jumla, fonimu za Kikamba ni ishirini na sita.

Utafiti umebainisha kuwa lugha ya Kikamba ina muundo wa silabi wazi. Vile vile, utafiti umetambua vipengele viwili vya fonolojia arudhi ambavyo ni silabi na neno. Tunatambua viwango viwili vya shada: shada silabi na shada neno.

Utafiti umebainisha kuwepo kwa mahusiano ya vigezo vya fonolojia ya Kikamba. Kuna uhusiano mkubwa baina ya silabi na sifa arudhi. Pia kuna uhusiano kati ya shada na silabi. Kuna kanuni zinazoongoza maumbo ya silabi na muundo wa fonimu. Kwa jumla, vipashio vya kifonolojia vinahusiana na kushirikiana katika muundo na uamilifu. Mahusiano hayo yanaweza kutumika katika utohozi fonolojia.

Sura hii pia imeonyesha uwiano uliopo kati ya lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia vipengele vya kifonolojia. Vibadala vya vipengele hivi vya kifonolojia katika lugha ya Kikamba ikilinganishwa na Kiswahili vilibainishwa; vibadala vya vokali, vibadala vya konsonanti na vibadala vya silabi.

SURA YA NNE

TARATIBU ZA UTOHOZI FONOLOJIA

4.1 Utangulizi

Utafiti huu unategemea ukweli kwamba maneno mkopo hayana budi kutoholewa ili kuafiki vigezo bayana vya sarufi ya lugha inayokopa. Utohozi unaweza kuchunguzwa kutegemea vigezo bayana vya kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki (Mwihaki, 1998). Sura hii inazingatia utohozi wa vigezo vya fonolojia ya lugha kopeshi na vile vya lugha inayokopa kupitia vigezo vya kifonolojia : fonimu, silabi na arudhi. Kama ilivyotajwa hapo awali, neno linapokopwa linaweza kukiuka muundo wa silabi za lugha kopaji na pia linaweza kuwa na fonimu zisizopatikana katika msamiati wa lugha kopaji. Lugha pokezi basi inakuwa na changamoto la kushughulikia muundo wa silabi hizo na fonimu hizo ngeni ili zikubaliane na zile za lugha kopaji.

4.2 Utohozi fonimu

Utohozi fonimu unarejelea mabadiliko ya fonimu za lugha kopeshi (Anttila, 1972). Fonimu zisizopatikana katika lugha inayokopa hulazimika kugeuzwa ili ziafiki kanuni za muundo husika wa kifonolojia. Fonimu zinabadilishana na zile ambazo zina uhusiano wa kifonetiki. Fonimu ambazo zinafanana kifonetiki hudumishwa (Mwihaki, 1998). Dhana ya udumishaji humaanisha kwamba kuna fonimu zinazofanana katika lugha kopaji na lugha kopeshi. Fonimu zinachukuliwa kufanana iwapo zina sifa sawa za kifonetiki. Uchunguzi wetu umezingatia utohozi wa fonimu za vokali na konsonanti.

4.2.1 Utohozi vokali

Vokali ambazo hutoholewa katika Kikamba ni mbili: /u/ na /i/. Vokali ya juu-mbele /i/ hujitokeza kama vokali ya kati mbele /e/ katika mazingira fulani. Mifano ifuatayo inabainisha mabadiliko hayo.

/i/ > /e/

Kiswahili		**Kikamba**
/kiatu/	>	/keato/
/kitamba:/	>	/ketamba:/
/kiɟikɔ]/	>	/kesikɔ/

Mabadiliko haya husababishwa na ukuruba mkubwa wa kifonetiki baina ya vokali hizi kutegemea mlalo wa ulimi. Zote ni sauti za mbele, tena sauti tandazi. Vile vile, vokali /i/ na /e/ zina uhusiano unaotokana na mwinuko wa ulimi; moja inafuata nyingine yaani vokali /i/ ni ya juu mbele nayo /e/ ni vokali ya kati mbele. Ujirani huu husababisha mabadiliko hayo. Katika mazingira mengine, vokali /i/ hudumisha umbo lake kwa mfano vijiko - /isikɔ/. Kwa hivyo sauti /i/ hugawika mara mbili kama inavyowakilishwa na kielelezo kifuatacho.



Vokali ya nyuma na juu /u/ hubadilika na kuwa ya nyuma na kati /o/ kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

Kiswahili		**Kikamba**
/mwalimu/	>	/mwalimo/
/kitungu:/	>	/ketoŋgo:/
/simu/	>	/simo/
/pingu/	>	/mbeŋgo/
/kalamu/	>	/kalamo/

Mabadiliko haya yamesababishwa na uhusiano wa kifonetiki baina ya vokali hizi. Vokali /o/ na /u/ ni za nyuma na tena ni sauti viringe. Katika baadhi ya nomino, vokali /u/ hudumisha umbo lake na hivyo inaweza kwa mfano kugawika mara mbili kama inavyodhihirika katika kielelezo hiki.



Kama ilivyodokezwa awali, lugha ya Kikamba ina vokali saba ilhali ya Kiswahili ina vokali tano. Utohozi vokali unategemea hitilafu hizi. Kupitia utohozi vokali, imebainika kuwa utohozi unahusisha konsonanti pia.

4.2.2 Utohozi wa Konsonanti

Mabadiliko katika maneno mkopo ya Kikamba yanasababishwa na tofauti zilizopo kati ya konsonanti za Kikamba na zile za Kiswahili.

Lugha ya Kikamba haina konsonanti zifuatazo: /p/, /f/, /d/, /ɟ/, /Φ/, /ð/, /z/, /h/, /r/,/b/, /g/, /ʃ/. Kwa hivyo lugha hii inapokumbana na sauti hizo ngeni huzigeuza na kuzifanya zitamkwe kama zile za Kikamba.

Uchunguzi umedhibitisha kwamba kipasuo /p/ hubadilika na kuwa kikwamizwa /÷/ au kizuiwa /mb/ katika utohozi wa maneno. Mifano ifuatayo inadhihirisha jambo hilo.

Kiswahili		**Kikamba**
/pesa/	>	/mbɛsa/
/pasi/	>	/÷asi/
/pamba/	>	/÷amba/
/papai/	>	/e÷a÷ai/
/pete/	>	/mbɛtɛ/
/pingu/	>	/mbeNgu/

[P] > [÷] na [P] > [mb]

Kwa kuwa lugha ya Kikamba haina konsonanti /p/, inapokumbana na neno lenye sauti hii huibadilisha na kuwa /÷/ au /mb/. Hivyo konsonanti /p/ inaweza kugawika mara mbili kama inavyoonyeshwa katika kielelezo hiki:-



Kipasuo /p/ hugeuka na kuwa kikwamizo /÷/ kutokana na ukuruba wa kifonetiki unaohusu pahali pa kutamkia. Konsonanti zote zinatamkiwa midomoni na hivyo huweza kubadilika katika mazingira yoyote kama vile mwanzo au katikati.

Katika lugha ya Kikamba, kipasuo /d/ hubadilishwa na kipasuo /nd/ au kipasuo /t/. Sauti hizi mbili zote ni vipasuo vya ufizi na hii ndiyo sababu ya kuwezesha mabadiliko haya.

Kwa mfano:

Kiswahili		**Kikamba**
/dawa/	>	/ndawa/
/duka/	>	/nduka/
/dErEva /	>	/ndElE÷a/
/daktari/	>	/ndaketale/
/darubini/	>	/ndolo÷Eni/

/faida/ > /÷aita/

/bidi:/ > /÷iti:/

[d] > [nd]

[d] > [t]

Kwa hivyo, kipasuo /d/ huweza kugawika kuwili ili kusilimishwa katika lugha ya Kikamba kama inavyoonyeshwa katika kielelezo kifuatacho.



Vile vile, kikwamizwa /f/ hubadilishwa na kuwa kikwamizwa /÷/.

Kiswahili		**Kikamba**
/faida/	>	/÷aita/
/faini/	>	/÷aine/
/[fundi/	>	/÷undi/
/[fulana/	>	/÷ulana/

Mabadiliko ya kikwamizo cha mdomo na meno /f/ kuwa kikwamizo cha mdomoni /÷/ yanasababishwa na sifa za kifonetiki pamoja na jinsi ya kuzitamka kwani sauti zote ni vikwamizo. /f/ > /÷/

Pia kikwamizo cha mdomo wa chini na meno ya juu /v/ hubadilika na kuwa kikwamizo cha midomoni /÷/.

Kwa mfano:

/mwavuli/	>	/mwa÷ule/
/v/	>	/÷/

Kipasuo /g/ hubadilika na kuwa kipasuo /ŋg/ au /k/. maneno yafuatayo yanadhihirisha mabadiliko hayo.

Kiswahili		**Kikamba**
/gari/	>	/ŋgale/
/gilasi/	>	/ŋgilasi/
/gunia/	>	/ekunia/
/godoro/	>	/ekɔndɔlɔ/

Kwa hivyo, /g/ hugawika kuwili katika nomino za Kikamba.



k

Kikwamizwa /Φ/ hugeuzwa na kuwa kipasuo /k/ au /ŋg/.

Kwa mfano:

Kiswahili		**Kikamba**
/Φarama/	>	/ŋgalama/
/Φɔrɔfa /	>	/ŋgɔlɔ÷a/
/Φasia/	>	/kasia/
/luΦa/	>	/loka/
/Φali/	>	/kale/

Kutokana na mifano hii, sauti /Φ/ hugawika mara mbili katika Kikamba:



Maneno yaliyo na kikwamizwa /h/ yanaposilimishwa hudondoshwa sauti hii ya /h/. Hii ni kwa sababu lugha ya Kikamba haina sauti za kooni (glota). Mifano ifuatayo inadhihirisha ukweli huu.

Kiswahili		**Kikamba**
/sahani /	>	/sa:ni/

/ruhusa/ > /lo:sa/

/sahihi/ > /sai:/

/mkahawa/ > /moka:wa/

/mtihani/ > /mtiane/

/mʃahara/ > /mosa:la/

/mhindi/ (mtu) > /moindi/

/mahamri/ > /ma:muli/

Kizuiwa – kwamizwa /ɟ/ hugeuzwa kuwa nusu-irabu /j/. Mfano mzuri unajitokeza katika majina ya siku.

Kiswahili **Kikamba**

/ɟumapili/ > /juma: ÷ele/

/ɟumatatu/ > /juma:tato/

/ɟumamosi/ > /juma:mɔsi/

/IɟumaːI/ > /juma:/

/ɟumatanɔ/ > /juma:tanɔ/

Mifano zaidi ni katika nomino zifuatazo.

/ɟEla/ > /jEla/

/mɟumbE/ > /mojumbE/

Kizuiwa /b/ husilimishwa na kuwa kikwamizwa /÷/ au kizuiwa /mb/. Mabadiliko haya huwezekana kutokana na sababu kwamba zote ni konsonanti za midomoni.

Kiswahili		**Kikamba**
/bidii/	>	/÷iti:/
/bahati /	>	/÷a:ti/
/bakuli /	>	/mbakoli/
/birika/	>	/mbilika/
/mabati/	>	/ma÷ati/
/sa÷atɔ/	>	/sa÷atɔ/
/bibilia/	>	/mbi÷ilia/
/baiskEli/	>	/÷asikili/
/zaburi/	>	/sa÷ule/
/bEndEra/	>	/ke÷EndEla/
/mzabibu/	>	/mosa÷i÷o/

Kutokana na mifano hii, uchunguzi ulitambua kwamba kipasuo /b/ hugawika mara mbili kinapokopwa na kuingizwa katika nomino za Kikamba. Mabadiliko haya yanawezeshwa na ukuruba unaotokana na mahali pa kutamkia.

÷



Kikwamizwa ghuna cha ufizi /z/ hubadilika na kuwa kikwamizwa sighuna /s/. Mabadiliko hayo yanabainishwa hapa kwa mifano ifuatayo.

Kiswahili		**Kikamba**
/zaburi /	>	/sa÷ule/
/baraza /	>	/÷alasa/
/mzE:/	>	/mosE:/
/mandazi/	>	/mandasi/
/ubatizɔ/	>	/o÷atisɔ/
/mzungu/	>	/mosoŋgo/

Mabadiliko ya fonimu /z/ kuwa /s/ yanatokana na sifa za kifonetiki na jinsi zinavyotamkwa. Fonimu zote hutamkiwa kwenye ufizi na pamoja na hayo, /z/ na /s/ ni vikwamizwa. Tofauti iliyopo baina ya fonimu hizi mbili ni kuwa /z/ ni ghuna ilhali /s/ ni sauti sighuna. Mabadiliko ya fonimu hizi hutokea katika mazingira yote ya kifonetiki, iwe mwanzoni au katikati mwa neno.

Utafiti ulibainisha kwamba pia kuna maneno machache ya Kikamba ambapo /z/ hubadilika na kuwa /nz/ au /Π/.

Kiswahili	**Kikamba**

/zabibu]/ > /nza÷i÷o/

/zambarau/ > /nzambalao/

/nazi/ > /naΠi/

Kutokana na mifano hii, tulitambua kwamba nomino zenye fonimu /z/ zinapokopwa na kuingizwa kwenye lugha ya Kikamba kuna uwezekano wa fonimu hiyo kugawika mara tatu kama inavyoonyeshwa:



Maneno ya Kiswahili yenye kikwamizwa /ʃ/ yanapokopwa na kuingizwa kwenye lugha ya Kikamba, /ʃ/ hubadilika na kuwa /s/.

Kiswahili		**Kikamba**
/ʃetani/	>	/satani/
/ʃati/	>	/sati/
/ʃiliŋgi/	>	/siliŋgi/
/maʃìndanɔ/	>	/masindanɔ/
/mʃahara/	>	/mosa:la/
/mʃìpi/	>	/mosi÷i/

Mabadiliko haya yanatokana na mambo mawili: sifa za kifonetiki na jinsi sauti hizi zinavyotamkwa. Sauti /ʃ/ hutamkiwa kwenye kaakaagumu na /s/ hutamkiwa kwenye ufizi. Kwa vile lugha ya Kikamba haina sauti /ʃ/, inapokumbana na sauti hii huitamka sawa na ile inayoikaribia, yaani /s/. Sauti hizi zote ni vikwamizo na mabadiliko haya hutokea katika mazingira yoyote, mwanzoni au katikati mwa neno.

Kimadende /r/ hubadilishwa na kuwa kitambaza /l/ kutokana na sifa za kifonetiki. Kwa mfano:

Kiswahili		**Kikamba**
/mpira]/	>	/mo÷ela/
/daktari/	>	/ndaketale/
/randa/	>	/landa/
/rangi/	>	/laŋgi/
/kaburi /	>	/ka÷ule/

Mabadiliko haya hutokana na sababu kwamba sauti /l/ na /r/ hutamkiwa kwenye ufizi na sauti zote mbili ni vilainisho. Hili linamaanisha kwamba konsonanti hizi hushiriki ukuruba wa kifonetiki wa kadiri kubwa.

Utohozi ulioelezwa unahusisha uunganifu wa fonimu. Vielelezo vifuatavyo ni mifano ya uunganishaji wa fonimu.

(i) Uunganishaji wa /l/ na /r/



(ii) Uunganishaji wa /s/, /z/ na /ʃ/



Sauti /s/, /ʃ/ na /z/ huungana kuwa fonimu moja /s/. Mabadiliko haya yanaonekana kudhibitiwa na kanuni fulani ambayo inahusu sifa za kifonetiki na jinsi zinavyotamkwa. Sauti zote zina uwiano wa pahali pa kutamkia na pia ni vikwamizo.

(iii) Uunganishaji wa /b/ na /p/



Sauti /b/ na /p/ huungana kuwa fonimu moja /÷/. Hii ni kwa sababu sauti zote zinatamkiwa midomoni.

Pia sauti /p/ na /b/ huweza kuungana na kuunda fonimu moja ya nazalishi awali /mb/ kama vile katika neno ‘mbete’ (pete) na ‘mbakuli’ (bakuli).



(iv) Uunganishaji wa /ʃ/ na /tʃ/



Kwa mfano

mchele – *musele* /mosElE/

shilingi – *silingi* /siliŋgi/

(v) Uunganishaji wa /p/, /v/, /f/ na /b/



/p/ na /b/ ni sauti za midomoni nazo /f/ na /v/ ni sauti za midomo-meno.

Ni muhimu kutambua kwamba ‘v’ ya kiothografia ya Kikamba haitamkwi kama kizwamizwa ghuna cha mdomo-meno /v/ bali hutamkwa kama kikwamizo sighuna cha midomoni (÷). (Kitavi, 1992).

4.3 Utohozi Silabi

Lugha nyingi hasa za Kibantu hutumia silabi wazi. Lugha ya Kikamba ikiwa lugha ya Kibantu, hutumia muundo wa silabi wazi ambayo humalizika kwa sauti ya vokali. Utohozi silabi huhusu mabadiliko katika maumbo husika. Chanzo cha mabadiliko katika silabi ya Kikamba hutokana na hitilafu kati ya maumbo ya silabi zake na yale ya Kiswahili. Lugha ya Kikamba haina muundo wa silabi za konsonanti pekee kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Maneno yaliyo na muundo huo yanapoingizwa katika lugha ya Kikamba husilimishwa ili yafuate muundo wa konsonanti – irabu (KI). Mabadiliko ya umbo la silabi yanayohusu Kikamba na Kiswahili hutegemea uchopekaji kati wa vokali katika neno.

Uchopekaji kati huja baada ya silabi ya konsonanti pekee ambayo katika Kiswahili ni nazali /m/. Lugha ya Kikamba inapokumbana na silabi ya /m/, huchopeka vokali ya nyuma na kati /o/ baada ya konsonanti /m/ ili kubadilisha umbo hilo liwe la silabi wazi yaani KV. Uchopekaji kati wa vokali /o/ unadhihirika katika mifano ifuatayo.

Mifano ya uchopekaji kati wa vokali /o/.

/m/ > /mo/

Kiswahili		**Kikamba**
mpira	>	mo$÷e$la

mkatɛ > mokatɛ

m$kɛ$bɛ > mo$kɛ÷ɛ

mfukɔ > mo$÷u$kɔ

m$kɛ$ka > mo$kɛ$ka

msumɛ$nɔ > mo$su$mɛ$nɔ

m$ʃi$pi > mosi÷i

mswaki > moswaki

mtuŋgi > motoŋgi

mpaka > mo$÷a$ka

Kupitia uchopekaji wa vokali /o/ baada ya nazali /m/, tunaweza kudai kwamba umbo silabi la /m/ (K) limetoholewa na kuwa umbo la konsonanti-irabu (KI). Sheria ifuatayo inahusika: k > KI.

Kwingineko, vokali /i/ au /e/ huchopekwa baada ya konsonanti. Tazama mifano ifuatayo:

Mifano ya uchopekaji wa vokali /i/ na /e/

Kiswahili **Kikamba**

/daktari/ > /ndaketali/

/mstari / > /mositale/

/bastɔla/ > /÷asitɔla/

Utafiti unatambua kwamba maneno ya Kiswahili katika utohozi huu yamejumuisha silabi za umbo la KVK. Hili ni umbo la silabi funge ambalo halikubaliki katika fonolojia ya Kikamba. Kwa hivyo, ili kurekebisha umbo hili, Kikamba huchopeka vokali /i/ au /e/. Urekebishaji wa u,mo la silabi unaenda sambamba na kuongezeka kwa idadi ya silabi katika kila neno. Utohozi silabi kwa hivyo mara nyingi unaenda pamoja na utohozi arudhi.

4.4 Utohozi arudhi

Utohozi arudhi unahusu mabadiliko ya idadi ya silabi kupitia kuweka kiambishi cha vokali mwanzoni mwa neno. Katika utohozi, nomino za Kiswahili zilizo katika ngeli ya LI-YA zinapokopwa na lugha ya Kikamba hulazimika kuwekwa kiambishi cha vokali /e/ ili dhana ya ukubwa ijitokeze. Nyingi za nomino hizi huwa ni vifaa vya kawaida na majina ya matunda.

Mifano ya uambishi wa vokali /e/, awali.

Kiswahili **Kikamba**

gunia > ekuni$a

sahani	>	esaa$ni
dɛ$bɛ	>	e$lɛ$÷ɛ
kɔ$ti	>	e$kɔ$ti
ba$ti	>	e$÷a$ti
gondorɔ	>	ekondɔ$lɔ
tu$nda	>	etunda
ɛ$mbɛ	>	e$ɛ$mbɛ
ʧu$ŋgwa	>	esuŋgwa
papai	>	e$÷a$÷ae
nanasi	>	enana$si
kanisa	>	ekani$sa
ri$nda	>	elinda

4.5 Hitimisho

Sura hii imeandikwa kwa madhumuni ya kubainisha taratibu zilizotumiwa katika utohozi fonolojia wa maneno mkopo ya Kikamba. Utafiti huu umetegemea data kwamba maneno hayana budi kutoholewa ili kuafiki vigezo bayana vya sarufi ya lugha ya Kikamba. Utohozi umezingatia utohozi fonimu, utohozi silabi na utohozi arudhi.

Utohozi fonimu ni utaratibu wa kubadilisha sauti bayana za lugha kopeshi na kuzipa muundo wa lugha inayokopa ili kuafiki sarufi ya lugha hiyo. Chanzo cha utohozi ni hitilafu ambazo zilipelekea fonimu za fonolojia ya Kiswahili kubadilishwa ili zilingane na zile za fonolojia ya Kikamba. Utohozi fonimu unajumuisha vokali na konsonanti.

Utohozi vokali umedhihirisha kwamba vokali zinazotoholewa ni mbili yaani /u/ na /i/ ambapo vokali ya juu-mbele /i/ hujitokeza kama vokali ya kati-mbele /e/ nayo vokali ya nyuma-juu /u/ hubadilika na kuwa ya nyuma-kati /o/. Mabadiliko haya yamesababishwa na uhusiano wa kifonetiki baina ya vokali hizi.

Utohozi konsonanti umedhihirisha kwamba kuna hitilafu kubwa baina ya konsonanti za Kikamba na zile za Kiswahili. Utohozi ulihusisha mbinu za uunganishaji konsonanti ambapo konsonanti tofauti ziligeuka na kuchukua umbo la fonimu moja. Baadhi ya konsonanti ziligawika maradufu na hata zaidi zilipotoholewa. Utohozi uliongozwa na kanuni na sheria za fonolojia ya Kikamba kupitia sifa mbalimbali za kifonetiki. Sifa hizo zinahusu jinsi na mahali pa kutamkia.

Sura hii pia imezingatia utohozi silabi ambao ulihusisha uchopekaji wa vokali baada ya nazali /m/, na pia baada ya konsonanti nyingine kama vile /s/ na /k/. Utohozi silabi unategemea kuwemo kwa baadhi ya maumbo silabi kama vile m na KVK ambayo

hukaidi kanuni za fonolojia ya Kikamba. Kanuni za sarufi ya Kikamba basi ndizo ziliongoza utohozi huu. Utohozi silabi uliandamana na utohozi arudhi.

Utohozi arudhi ulihusisha mbinu ya uambishi wa vokali mwanzoni mwa neno. Uambishi ulitumia vokali moja ambayo ni /e/. Vokali hii huwa silabi kamili ikiwa katika mazingira ya mwanzo wa neno. Kwa hivyo vokali hii inapochopekwa kwenye maneno ya Kikamba, husababisha umbo asilia la neno kubadilika kupitia kuongezeka kwa idadi ya silabi zake. Utohozi uliongozwa na kanuni na sheria za fonolojia ya Kikamba. Sifa kuhusu muundo wa maumbo ya silabi na sifa mbalimbali za kifonetiki zilihusika.

Kuna uhusiano mkubwa katika mabadiliko ya silabi na idadi ya maumbo na silabi yenyewe. Tunaweza kutoa kauli kwamba wasemaji wa lugha ya Kikamba huwa na ujuzi asilia wa kugeuza maneno mkopo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Uchunguzi huu ulifanywa kutekeleza madhumuni ya kuchanganua na kutathmini kanuni za kifonolojia zinazotumika katika utohozi wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Nadharia ya Fonolojia ya vipande sauti huru ilitumiwa katika kazi hii kwa sababu ni nadharia ya kisasa inayotazama mfumo sauti kama rusu. Nadharia hii hueleza rusu kama mpangilio wa vipande huru vya kifonolojia vinavyohusiana na kujengana. Vipande hivi vinaweza kutenganishwa na kutazamwa pekee bila kuhusishwa na kingine. Nadharia ya mawimbi pia ilitumiwa kufafanua sababu za kiisimu jamii zilizochangia ukopaji wa maneno katika Kikamba. Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti wetu, mahitimisho na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

5.2 Muhtasari

Utafiti umeonyesha sababu za kiisimu jamii zilizochangia ukopaji wa maneno katika lugha ya Kikamba kutoka Kiswahili. Sehemu hii ni muhimu katika kazi yetu kwani inatofautisha kazi yetu na tafiti za awali zilizoshughulikia maneno mkopo. Uchunguzi huu pia umeshughulikia taratibu za utohozi fonolojia ambapo mbinu kuu zinazotumia ni udondoshaji, uchopekaji na pia ugeuzaji maumbo unaosababisha udhoofishaji wa sauti. Ulinganishi wa fonolojia baina ya lugha ya Kiswahili na Kikamba umefanywa na kufafanua vibadala vya vokali na vile vya konsonanti kati ya lugha hizi. Mbinu za utafiti

zilizohusishwa ni mbili: utafiti wa maktabani na ule wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulifanywa kwa udurusu wa vitabu mbalimbali, tasnifu, machapisho na majarida. Mbinu hii ilikuwa na manufaa katika utafiti huu kwa kuchangia ufahamu wa nadharia zilizotumiwa katika tafiti za awali. Pia, kupitia mbinu hii, pengo lililohitaji kutafitiwa lilibainika. Utafiti wa nyanjani ndio ulihusika zaidi katika utafiti huu kwa sababu uliangazia mambo halisi ambayo hayawezi kumulikwa na utafiti wa maktabani. Utafiti wa nyanjani ulilenga kutambua data ya manenomkopo, uchanganuzi na uwasilishi wa data.

Manenomkopo yalitambuliwa kwa kulinganisha leksia kutoka lugha changizi na lugha pokezi ambazo ni Kiswahili na Kikamba mtawalia, kutegemea tamaduni za lugha hizi. Data ilikusanywa kupitia uchunguzi wa kushiriki. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuchunguza vigezo vilivyobadilika pamoja na taratibu zilizotumiwa katika utohozi. Data iliwasilishwa kwa maelezo na udhihirishaji wa kisayansi kama vile majedwali na michoro matawi.

5.3 Matokeo ya utafiti

Utafiti wetu umethibitisha kwamba kuna maneno ya mkopo yanayodhihirika katika Kikamba cha Kitui ya kati yanayotokana na lugha ya Kiswahili ambayo ina uamilifu wa lugha ya taifa na pia lugha sambazi. Vile vile, imebainika wazi katika utafiti huu kwamba kuna sababu nyingi za kiisimu jamii zilizopelekea Kikamba cha Kitui ya kati kukopa maneno kutoka Kiswahili. Kama wanavyotambua wana isimu jamii, lugha

zinapoingiliana huathiriana. Kwa kawaida, lugha inayokopa ni ile yenye hadhi ya chini ikilinganishwa na lugha inayokopesha ambayo huwa ya hadhi ya juu (Mwita, 2009). Jambo hili limesababisha kuhifadhiwa kwa baadhi ya vipashio vya lugha kopeshi.

Aidha, maneno mkopo yamewezesha kukua kwa lugha ya Kikamba na kuongezeka kwa uwezo wa kutekeleza majukumu yake. Kwa kiwango fulani, kukopa msamiati kutoka kwa Kiswahili kumefanya lugha ya Kikamba kutoka katika kambi ya kawaida na kuzidi kuwa na umahususi. Kwa mfano, badala ya kuwa na jina moja la baiskeli kama zilivyo baadhi ya lugha, lugha hii ina sinonimu ‘vasikili’ na ‘kisululu’. Kukua ni miongoni mwa sifa za kimaumbile za kitu chochote kilicho na uhai na maadam lugha ihai, ndio maana lugha hii imekopa maneno mbalimbali yanayokidhi mahitaji mapya yanayozuka.

Uchunguzi wetu ulitambua kwamba Fonolojia ya Kikamba inategemea mfumo wa konsonanti kumi na tisa na vokali saba. Kinyume na ilivyo katika vokali za Kikamba, konsonanti za Kikamba hazitumiki katika mazingira yoyote ya matumizi ya neno.

Mpangilio maalum wa vokali na konsonanti unamulika sifa za kifonetiki ambazo kwa kawaida huhusishwa na muundo wa fonimu nao muundo wa fonimu unamulika sifa maalum za kifonetiki zinazosawiri muundo wa silabi za Kikamba. Imebainika kuwa lugha ya Kikamba ina silabi wazi ambazo zina miundo tofauti. Pia, utafiti umebainisha ngazi tatu za utohozi: utohozi fonimu, utohozi silabi na utohozi arudhi.

Utohozi fonimu umedhihirisha mabadiliko ya fonimu za vokali na za konsonanti. Utohozi vokali na utohozi konsonanti umebainisha mazingira ya kifonetiki. Sifa hizi zinamulika uhusiano na utohozi silabi.

Utohozi silabi umebainisha uchopekaji wa vokali baina ya konsonanti mbili ili kurekebisha umbo la silabi ya Kiswahili lifanane na lile la Kikamba. Kwa kawaida, lugha ya Kikamba haina silabi funge. Maumbo mengi yaliyohusika ni yenye silabi ya konsonanti ya nazali /m/. Vokali inayochopekwa baina ya silabi ya nazali /m/ na ile inayofuata ni /o/. Kwa mfano mti – mote. Uchopekaji wa vokali /i/ ulitambuliwa katikati ya konsonanti nyingine zisizokuwa za nazali. Kwa mfano mstari – mositale, daktari – ndaketale.

Utohozi arudhi umedhihirisha uambishi mwanzo wa vokali kwenye maneno ya Kikamba. Vokali /e/ huwekwa mwanzoni mwa maneno ya Kiswahili yaliyo katika ngeli ya li – ya. Kwa mfano, gunia – ekunia, sanduku – esanduku. Hii ni kwa sababu katika Kikamba, nomino katika hali ya ukubwa huanza kwa vokali /e/. Kwa mfano mundu –[emundu] (jitu), ngua – [ekula] (guo).

Utafiti ulitambua kwamba lugha ya Kikamba haina wakaa mrefu na badala yake kila mfuatano wa vokali huchukuliwa kama silabi inayojitegemea. Vile vile, lugha ya Kikamba hupendelea sana sauti sighuna kuliko zile ghuna. Hii ndiyo sababu iliyopelekea udhoofishaji wa konsonanti zinazopatikana katika maneno ya Kiswahili zinapokopwa na kuingizwa katika Kikamba. Kwa mfano: mEza - mEsa.

Muhtasari wa matokeo kwa jumla unaonyesha kwamba vigezo mbalimbali hutawaliwa na kanuni bayana. Kwa upande mwingine, vigezo vya fonolojia ya Kikamba vinafaa kama msingi wa uchanganuzi toshelevu wa mabadiliko katika utohozi wa manenomkopo.

5.4 Mahitimisho

Sehemu ya mahitimisho inajumuisha kigezo cha fonimu, silabi na sifa arudhi. Utohozi vokali haukuonyesha hitilafu kubwa baina ya vokali za Kikamba na zile za Kiswahili. Huu ni ushahidi kwamba lugha hizi mbili zina ukuruba mkubwa wa kifonetiki. Vokali zinazofanana katika lugha ya Kikamba na ya Kiswahili hugeuka kutegemea mazingira fulani katika neno. Utohozi vokali umedhihirisha kwamba vokali zingine ziliathiriwa na konsonanti fulani zilizo karibu.

Utohozi konsonanti ulitegemea hitilafu kubwa kati ya konsonanti za Kikamba na zile za Kiswahili. Mabadiliko ya konsonanti yanahusu kugawika kwa konsonanti, uunganishaji na ugeukaji. Ugavi wa konsonanti unahusu konsonanti moja inayobadilika na kuchukua maumbo tofauti tofauti. Uunganishaji konsonanti ni mabadiliko yanayofanya konsonanti mbalimbali kuchukua umbo moja. Kuhusu ugeukaji, kuna konsonanti zinazogeuka na kuchukua umbo la konsonanti iliyo karibu nayo kulingana na sifa za kifonetiki. Baadhi ya konsonanti zinazopatikana katika lugha zote mbili ziligeuka katika mazingira fulani. Hata hivyo, utohozi uliongozwa na sifa za jinsi na pahali pa kutamkia. Utohozi fonimu uliowakilishwa unaonekana kuwa na mahusiano na utohozi silabi.

Uchunguzi umebainisha kuwa lugha ya Kikamba husawiri muundo wa silabi wazi. Kutokana na muundo huu, imebainika kwamba nomino zote za Kikamba huchopeka vokali baada ya konsonanti ili kuafiki muundo wa silabi wazi. Vokali iliyochopekwa kwa wingi ni /o/. Vokali /i/ pia ilitumika mara chache hasa baada ya /k/ na /s/, Utohozi silabi ulionekana kwenda sambamba na utohozi arudhi kutokana na uchopekaji wa vokali mwanzo; ambao unaongeza idadi ya silabi katika neno.

Kutokana na matokeo ya utafiti, imebainika kwamba utohozi arudhi husababisha idadi ya silabi kuongezeka kutokana na uchopekaji mwanzo wa vokali katika maneno ya Kikamba. Vokali iliyochopekwa mwanzoni mwa maneno ya Kikamba ni /e/ hasa kwenye nomino mbalimbali zilizo katika ngeli ya li – ya ya Kiswahili. Matokeo na mahitimisho ya utafiti yamebainisha kuwepo na maswala kadhaa yanayohitaji kufanyiwa utafiti.

5.5 Mapendekezo

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Fonolojia ya vipande sauti huru kuchunguza manenomkopo ya Kikamba. Uchunguzi umebainisha kwamba utohozi unahusu fonimu, silabi na toni lakini utafiti huu haukushughulikia swala la toni. Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha jinsi ambavyo toni inahusika katika utohozi wa maneno kwani Kikamba ni lugha toni.

Uchunguzi umejikita katika maneno mkopo ya Kikamba yaliyotoka kwenye lugha ya Kiswahili. Imetajwa awali kwamba lugha ya Kikamba imekopa maneno kutoka lugha nyingine kama vile kiingereza na lugha nyingine za Kiafrika. Utafiti unahitajika kuchunguza manenomkopo ya Kikamba yaliyokopwa kutoka lugha hizi nyingine.

Ukopaji ni wa aina nyingi na uchunguzi huu umeshughulikia tu utohozi. Utafiti unahitajika kuchunguza maneno ya Kikamba yaliyokopwa kutoka Kiswahili kwa njia ya tafsiri mkopo au pia ukopaji wa sisisi. Vile vile, tafiti nyingine zinahitajika kuchunguza utohozi kutegemea viwango mbalimbali kama vile sintaksia, mofolojia na semantiki.

Pia, kuna uwezekano kwamba maneno asilia ya Kikamba yanabadilishwa na maneno mkopo kutokana na hadhi inayopatikana katika lugha kopezi. Utafiti wa kiulinganishi unahitajika kufanywa kuhusu matumizi ya maneno mkopo baina ya vijana na wazee.

Vile vile, uchunguzi wetu umeshughulikia nomino pekee. Utafiti unapaswa kufanywa kuhusu kategoria zingine za maneno mkopo ya Kikamba kama vile vitenzi na vivumishi.

Wizara ya Elimu nchini Kenya husisitiza matumizi ya lugha ya kwanza katika kufunza miaka ya kwanza mitatu katika shule za msingi (Kioko na Muthwii 2001). Utafiti wetu unapendekeza uhakiki ufanyiwe vitabu vinavyotumiwa kufunza Kikamba ili vijumuishe maneno mkopo ambayo kwa sasa ni mengi katika msamiati wa Kikamba.

Vile vile, tunapendekeza wanaotafsiri pamoja na wakalimani hasa wanaotafsiri kazi za Kiswahili hadi Kikamba watumie matokeo ya utafiti huu. Pia watangazaji na wanahabari wa idhaa za Kikamba wanaokumbana na maneno mapya kila siku wanaweza kutumia utafiti huu kwani umeeleza taratibu za usilimisho wa maneno mkopo ya Kikamba.

5.6 Hitimisho

Katika sura hii, muhtasari wa matokeo, mahitimisho na mapendekezo umefanywa. Sura hii pia imetoa mapendekezo ya tafiti zingine zinazoweza kufanywa kuhusu maneno mkopo ya Kikamba.

MAREJELEO

Antlila, R. (1972). *An Introduction to History and Comparative Linguistics.* New York: Macmillan.

Ball, M. E. (1971). Variations in the Assimilation of Arabic and English Loanwords into Kiswahili of Mombasa Kenya, PhD Thesis, University of Texas.

Bynon, T. (1977). *Historical Linguistics*. London: Macmillan.

Chomsky, N and M. Halle (1968). *The Sound Pattern of English*. New York: Harper & Publishers.

Chomsky, N and M. Halle (2005). Language Borrowing and Language Diffusion*:* An Overview in *Intercultural Communication Studies*. X1:4 200.

Goldsmith, J. A. (1990). *Autosegmental and Metrical Phonology*. Oxford: Basil Blackwell.

Guthrie, M. (1967). *The Classification of Bantu Languages*. London: Dawsons of Pall Mall.

Heinne, B. (1978*). A Typology of African Languages*. Berlin: Deitrich Reimer Verlag.

Hoofer, B. L. (2005). Language Borrowing and the Indices of Adaptability and Receptivity. In *Intercultural Communication Studies*, XIV: 2005

Houpe, D. W. (1978). Loanwords in Baraza: A Study of Lexical Origins in Kiswahili Language Newspapers, PhD Thesis University of Carolina.

Hyman, L. M. (1975). *Phonology: Theory and Analysis.* San Francisco: Holt, Rhinehart &

Winston, Inco.

Iribemwangi, P. I. (2012). Phonology of Borrowed Lexicon in Standard Kiswahili. In *Reyono Journal of Interdisciplinary Studies.* St. Thomas College, Kozhencherry, India. Vol. 1 No. 2. pp 59-74.

Iribemwangi, P. I 2013). Cultural Transfer from Europe and Asia to Africa: Evidence from Borrowed Lexicon Adapted into Kiswahili. *International Journal of Education and Research.* Vol. 1 No. 8. pp 1-14.

Johannes, S. (1872). The Relationship of Indo-Germanic Languages. Germany: University of Bonn press.

Kioko, A. N. and Muthwii, M. J. (2001*).* The Demands of a changing Society: English in

Education in Kenya today. In *language, Culture and Curricullum*, Vol. 14 No. 3.

Kitavi, H. M. (1992). A Comparative Study of the Kitui and Machakos Dialects of Kikamba. Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta ambayo haijachapishwa.

Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics*. New York: Cambridge University Press.

Mathooko, P. M. (2004). A Integrated Perspective of Language Accomondation*:* A Case Study of Kitharaka na Kikamba, An Unpublished PhD Thesis, Kenyatta University.

Maundu, P. M. (1980). Sound Change and the Reconstruction of Kikamba Consonantal Sounds in Natural Generative Phonology Framework. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbaabu, L. (1996). *Language Policy in East Africa: A Dependancy Theory Perspective.* Nairobi; General Printers Ltd.

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi; Longhorn Publishers.

Mohammed, M. A.(2001). Modern Swahili Grammar. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mugenda, A. G. (2008). *Social Science Research: Theory and Principles.* Nairobi: Acts Press.

Mugenda, O. and Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative approaches*. Nairobi: Acts Press.

Muhati, P. (2000). Matatizo ya Kuelewana Kimaongezi miongoni mwa Wabaluhyia wa Magharibi mwa Kenya Wanaozungumza Lahaja za Kiisukha, Kikisa, Kiloogoli na Kibukusu. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutiga, J. M. (2002). The Tone System of Kikamba: A Case Study of Mwingi Dialect. Tasnifu ya uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Mutisya, J. (1986). Concordial Agreement in Kiswahili and Kikamba, Unpublished PhD Thesis,University of Nairobi.

Mwihaki, A. N. (1998). Loanword Nativisation: A Generative View of the Phonological Adaptation of Gikuyu Loanwords, Doctoral Thesis, Kenyatta University.

Mwita, L. C. (2009). The Adaptation of Swahili Loanwords from Arabic: A Constraint-Based Analysis. In *the Journal of Pan African Studies,* Vol. 2 *No. 8, 46-60*

Ndambuki, B. M. (2013). A Constraint-Based Analysis of Kikamba Nativized Loanwords.

Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Newman, P. (2000). Comparative Linguistics in *D. Nurse and B. Heine (eds) African*

Languages: An Introduction: Cambridge University Press

Ngesu, S. N. (2004). "Usilimisho wa Maneno ya Mkopo Katika Lahaja ya Kikamba ya Mwingi."

Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njeru, M. D. W. (1990). Lexical Expansion in Kiswahili: A Study of Strategies in Corpus

Development. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Schane, S. A. (1973). *Generative phonology.* Eaglewood Cliffs: Prentice Hall.

TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu*, Dar-es-salaam: TUKI

Verma, S. K. and Krishnaswamy, N. (1989). *Modern Linguistics*. New York: Oxford University Press.

Waihiga, G. na K. W. Wamitila, (2003). *Chemchemi za Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Wald, B (1989). Swahili and the Bantu languages. *In B. Comrie (ed.) The World's major Languages:* London; Routledge.

Whiteley, W. H. and M. G. Muli, (1962). *Practical Introduction to Kamba*, London: Oxford University Press.

Whiteley, W. H. and M. G. Muli (1963). Loanwords in Kamba: A Preliminary Survey *African Language Studies, IV.*

Zawawi, S. (1974). Loanwords and Their Effect on the Classification of Swahili Nominals: A Morphological Treatment. PhD Thesis, University of Columbia.

KIAMBATANISHO

MANENOMKOPO YA KIKAMBA KUTOKA KISWAHILI

Orodha ifuatayo inaonyesha manenomkopo ya Kikamba yanayotokana na lugha ya Kiswahili. Orodha hii imeandikwa katika vitengo mbalimbali kutegemea maana za maneno hayo.

Kiutawala

Kiswahili		**Kikamba**	
askari	>	*asikali*	[asikale]
pingu	>	*mbingu*	[mbeŋgo]
jela	>	*yela*	[jEla]
kɔtini	>	*kotini*	[kɔtine]
baraza	>	*valasa*	[÷alasa]
polisi	>	*volisi*	[÷ɔlisi]
kapteni	>	*kavuteni*	[ka÷utEni]
wakili	>	*wakili*	[wakili]
bEndEra	>	*kivendela*	[ke÷EndEla]
kura	>	*kula*	[kula]

Mapambo

Kiswahili		**Kikamba**	
pete	>	*mbete*	[mbEtE]
rinda	>	*ilinda*	[elinda]
mshipi	>	*musivi*	[mosi÷i]
shati	>	*sati*	[sati]
fulana	>	*vulana*	[÷ulana]
mafuta	>	*mauta*	[mauta]
kofia	>	*ngovia*	[ŋgɔ÷ia]
suruali	>	*suluali*	[suluale]
koti	>	*ikoti*	[ekɔti]
kamisi	>	*kamisi*	[kamisi]
kiatu	>	*kiatu*	[keato]

Kitaaluma / zana za kazi

Kiswahili		**Kikamba**	
cherahani	>	*kyalaani*	[tʃala:ni]
simu	>	*simu*	[simo]

darubini	>	*nduluveni*	[ndolo÷Eni]
kalamu	>	*kalamu*	[kalamo]
fundi	>	*vundi*	[÷undi]
saa	>	*saa*	[sa:]
mutihani	>	*mutiani*	[motiane]
mwalimu	>	*mwalimu*	[mwalimo]
dawa	>	*ndawa*	[ndawa]
daktari	>	*ndakitali*	[ndaketale]
randa	>	*landa*	[landa]
rangi	>	*langi*	[langi]
msingi	>	*musingi*	[mosiŋgi]
msumeno	>	*musumeno*	[mosumEno]
mabati	>	*mavati*	[ma÷ati]
msumari	>	*musumali*	[mosumali]
sahihi	>	*saii*	[sai:]
mstari	>	*musitali*	[mositale]

Vyakula na lishe

Kiswahili		**Kikamba**	
mandazi	>	*mandasi*	[mandasi]
mkate	>	*mukate*	[mokatE]
chai	>	*kyai*	[tʃai]
mahamri	>	*mamuli*	[mamule]
mkahawa	>	*mukaawa*	[moka:wa]
mchele	>	*musele*	[mosElE]
sukari	>	*sukali*	[sukale]
machungwa	>	*masungwa*	[masuŋgwa]
nazi	>	*nathi*	[naΓIi]
ngano	>	*nganu*	[ŋgano]
mapapai	>	*mavavai*	[ma÷a÷ai]

Vyombo vya nyumbani

Kiswahili		**Kikamba**	
kijiko	>	*kisiko*	[kesikɔ]
mtungi	>	*mutungi*	[motoŋgi]
pasi	>	*vasi*	[÷asi]
gilasi	>	*ngilasi*	[ŋgilasi]
kitanda	>	*kitanda*	[ketanda]
gondoro	>	*ikondolo*	[ekɔndɔlɔ]
gunia	>	*ikunia*	[ekunia]
sahani	>	*saani*	[sa:ni]
bakuli	>	*mbakuli*	[mbakoli]
birika	>	*mbilika*	[mbeleka]
sindano	>	*sindano*	[sindanɔ]
mkebe	>	*mukeve*	[mokE÷E]
kikombe	>	*kikombe*	[kekɔmbE]
meza	>	*mesa*	[mEsa]
karai	>	*kalai*	[kalae]

chupa > *kisuva* [kesu÷a]

Dini

Kiswahili **Kikamba**

kanisa > *ikanisa* [ekanisa]

msikiti > *musikiti* [mosikiti]

bibilia > *mbivilia* [mbi÷ilia]

shetani > *satani* [satani]

zaburi > *savuli* [sa÷ule]

mzabibu > *musavivu* [mosa÷i÷o]

katoliki > *katholeki* [kaΠɔlEki]

sabato > *savato* [sa÷atɔ]

ubatizo > *uvatiso* [o÷atiso]

Biashara

Kiswahili **Kikamba**

pesa > *mbesa* [mbEsa]

gharama > *ngalama* [ŋgalama]

shilingi > *silingi* [siliŋgi]

biashara	>	*viasala*	[÷iasala]
risiti	>	*lisiti*	[lisiti]
ndururu	>	*ndululu*	[ndululu]
duka	>	*nduka*	[nduka]
bengi	>	*vengi*	[÷Eŋgi]

Vifaa vya michezo

Kiswahili		**Kikamba**	
kiwanja	>	*kiwanza*	[kewanza]
mpira	>	*muvila*	[mo÷ela]

Usafiri

Kiswahili		**Kikamba**	
gari	>	*ngali*	[ŋgale]
baiskeli	>	*vasikili*	[÷asikili]
tairi	>	*taili*	[taili]